
# النفس منطقة الخطر / السواحلية

SHEIKH: HASSAN MUSA SAFFAR



# NAFSI MAHALI PA HATARI

Imefasiriwa kutoka kwenye kitabu:

*An-nafsu mantaqatul-khatar'*

Sheikh Hassan Saffar

**YALIYOMO**

MLANGO WA KWANZA........................................ 1

SEHEMU YA HATARI........................................ 1

Maana ya Roho........................................ 1

Ni nini Akili?........................................ 2

Maana ya Nafsi........................................ 2

Tofauti ya Nafsi na Akili........................................ 2

Akili........................................ 2

Nafsi........................................ 3

Ni ipi kazi ya akili........................................ 3

Vipi akili hutekwa........................................ 4

Akili ni mateka, lakini kwa nani?........................................ 5

Pengo katika kueleza maana ya mantiki kwa wagiriki........................................ 6

Kutilia umuhumi juu ya nafsi........................................ 8

Wajibu wetu juu ya nafsi ........................................ 10

Mtazamo wa makosa........................................ 10

MLANGO WA PILI.......................................... 13

HATARI YA NAFSI KATIKA MANTIKI YA

KIISLAMU ................................................................ 13

Nafsi ni yenye kuamrisha maovu.................................. 13

JIHADI KUBWA-JIHADI DHIDI YA NAFSI......... 19

NAFSI NA ATHARI ZAKE ZILIZO WAZI KWA MWANAADAMU................................................ 25

MIONGONI MWA MARADHI YA NAFSI............ 26

KWANZA NI KUREKEBISHA NAFSI IWE

KATIKA NJIA YA SAWA........................................ 29

NAFSI NI ADUI ALIYE HATARI ZAIDI.............. 33

KUIHESABU NAFSI NA KUICHUNGA.............. 34

NATIJA YA KUPOTOKA KWA NAFSI................ 37

MLANGO WA TATU.............................................. 39

HATARI YA KUANGUKA KWENYE MAOVU....... 39

HATARI INATOKEA WAPI?....................................... 43

Mosi: Kufeli katika malezi........................................ 43

Pili: Shinikizo dhidi ya mafungamano ya kidini.......... 43

Tatu: Kuathirika na mazingira yaliyo haribika........... 44

Nne: na la mwisho: Kazi ya shetani.......................... 44

Tahadharini na maelekezo ya shetani......................... 45

WADHAMINI JUU YA KUWA NA MSIMAMO THABITI........................................................................ 49

Miongoni mwa wasia wa Mtume (s.a.w.)........................ 50

Miongoni mwa wasia wa kiongozi wa waumini (a.s.)........................................................................ 51

Miongoni mwa wasia wa Imam Hasan bin Ali (a.s.)........................................................................ 52

Miongoni mwa wasia wa Imam Muhammad Baqir (a.s.)........................................................................ 53

Miongoni mwa wasia wa Imam Jafar Sadiq (a.s.)........ 54

Katika wasia wa Imam Musa Al-Kadhim (a.s.)........... 57

## UTANGULIZI

Mwanadamu anafanya kila juhudi na uwezekano mkubwa kwa ajili ya umuhimu wa mwili wake na kutafuta maisha. Hadi imekuwa kila sehemu inayomuendeshea maisha yake kuwa na mtaalamu anaendesha au kusimamia nyanja hiyo. Kwa mfano: upande wa ulaji na vyakula- kuna ukulima, ufugaji wanyama na uvuvi pia. Na vyakula hutengezwa kwa sampuli mbalimbali kwa upande wa afya na utabibu. Kuna hospitali au zahanati, utengezaji wa madawa, utafiti wa maradhi na uvumbuzi wa madawa yake.

Vilevile katika upande wa mavazi na mapambo, vyombo ya nyumbani, mitindo (*fashion*) na urembeshaji, na katika haya pia kuna ujuzi mwingi na umuhimu mkubwa.

Na kwa kutilia umuhimu katika upande wa kiakili ya mwanadamu, watu wamepiga hatua kubwa katika uvumbuzi wa mambo walivyokuwa hawayafahamu kamwe ya elimu na ulimwengu kwa jumla. Na kila sehemu ya ujuzi ina fani yake na mvumbuzi wake. Kwa ajili hiyo kumekuwa na madrasa (shule) vyuo vikuuu, vyuo vya utafiti na elimu, Kongamano, mihadhara na hata magazeti na vitabu. Na bado shughuli za uvumbuzi wa maarifa na ujuzi ni zenye kuendelea na kufuatana kwa msururu.

Ama tukiangalia katika upande wa uroho wa nafsi, tunakuta kuwa ni kiungo kilichopuuzwa na kutotiliwa maanani katika watu wa mwanadamu ila kuna uchache tu. Hata katika usomeshaji wa ilmu ya nafsi umelemea sana katika upande wa kutafuta maisha ndipo maana asili ya roho imekuwa haijulikani.

Wala hatutakuwa tumekosa tunaposema kuwa ujumbe ulioletwa na Mitume na sheria za Mwenyezi Mungu katika dini yote haya yamekuja kutilia muhimu mambo ya kimsingi Kwanza kabla mengine kwa umuhimu ulioko. Na kwa kufahamu kwake Mwenyezi Mungu kuwa mwanadamu ni kiumbe dhaifu na mwingi wa kumsahau yeye ndipo Qur'an

ikaeleza malengo ya kutuilizwa Mtume (s.a.w.). Nayo ni kutakaswa kwa nyoyo na jambo hili limepewa kipaumbele.

Mwenyezi Mungu anasema katika *Suratil Jum'a* : "Yeye ndiye aliyeleta Mtume katika wasiojua kusoma, anaetokana na wao, awasome Aya zake na kuwatakasa na kuwafunza kitabu na hekima."

Na Mtume (s.a.w.w) kazi yake kubwa na iliyo muhimu ilikuwa ni kutayarisha na kukamilisha kustawi kwa roho au nafsi ambayo ndilo chimbuko la tabia ya mwanadamu. Amesema Mtume (s.a.w.) katika Hadith iliyo mashuhuri kwamba: "Hakika nimeletwa ili kutimiliza tabia njema."

Kwa ajili hiyo basi, hakika utajiri wa kiroho ni jambo kubwa na la umuhimu katika Uislamu. Lakini mwanadamu leo ameipoteza fursa hii akawa ni mwenye kufuata starehe na matamanio, sasa anachukulia kama kiumbe kilicho pweke na asiye maana.

Na haya kuwa machungu na mikasa ya kuhuzunisha inayomkabili mwanadamu ila ni matokeo ya kuwa mbali kwake na utakaso wa roho au nafsi. Mikasa yenyewe ni kama, uadui, ubanguzi wa rangi, ufukara, njaa na mauti, maovu yaliyoenea, uharibifu mkubwa wa kitabia, unyakuzi wa haki za watu na mengineyo.

Hakika iko haja kubwa leo kwa mwanadanu wakati wowote ule ya kuupata utajiri wa Uislamu kiroho na kupata mali ya kiislamu kimaana.. Na hapo ndipo inakuja nafasi ya Waislamu kuivumbua mali hiyo na kuiweka wazi kwa walimwengu wote ili wafaidike.

Masikitiko ni kwamba Waislamu wengi wameacha kujifunza sheria za dini na kuipuuza au kujitenga na dini yao. Hata wamekaribia kuwa sawa na wasio wao katika kutofahamu mafunzo ya dini yao, na wala hawafuati sheria za dini ila kwa uchache tu, huku wakishindana na wengine katika kuendelea kimali.

Hivyo basi, kwa ajili ya mwamko mpya wa kidini na kuendelea kwa Uislamu, ambao unavumia upande wa Waislamu. Imekuwa hapana budi na kutililia umuhimu katika kiungo hiki (roho) upande wa tabia ili kuendeleza utamaduni wa kiislamu.

Basi ewe msomaji, maandishi haya yaliyo mbele yako ni jaribio dogo tu katika kushirikiana ili kutilia umuhimu sehemu hii ya hatari.

Na katika ushahidi wa maneno haya kuna Hadith nyingi nimezieleza katika mihadhara tofauti nilioifanya sehemu tofauti. Na kwa kurikodiwa kwake zimepata umaarufu na kukubaliwa na wengi. Jambo ambalo limepelekea baadhi ya ndugu zetu wa kiislamu kuyaandika, kuchapisha na kueneza baada ya kufanyiwa marekebisho kidogo.

Mbali na urekebishaji kwanza natanguliza udhuru wangu kwa msomaji iwapo sikuweza kuchapa maneno haya katika njia au mtindo unaofaa.

Pia namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ni mwenye kufaidika na maneno haya. Na Ayajaaliye kuwa ya dhati kwa ajili yake na awanufaishe nayo Waislamu kwa jumla. Shukrani zote ni zake Mola kwa kutuneemesha na kutupa tawfiq (urahisi wa mambo).

Mtungaji

Hasan Saffar

1/8/1411 (A.H.)

# MLANGO WA KWANZA

## SEHEMU YA HATARI

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an Suratush Shamsi 7-10: "Naapa kwa nafsi na aliyetengeneza, kisha akaifahamisha uovu wake na ubaya wake. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa nafsi yake. Na bila shaka amejihasiri aliyeiviza nafsi yake."

Kuna vitu vitatu katika maisha ya mwanadamu. Na ni kutokana na ushirikiano wa utendaji kazi wa vitu hivi ndipo kunajengeka utu wa mwanadamu.

Vitu hivi ni:

1. Akili

2. Nafsi

3. Mwili au kiwiliwili.

Lakini yapasa tuelewe kuwa roho ndicho chambo ambacho kimekusanya vitu vitatu kwa jumla.

Pengine kuna umuhimu mkubwa juu ya kufafanua vitu hivi kimoja baada ya chengine. Kwanza ni nini roho? Na ni nini Akili? Na nafsi ni nini?

Ama kiwiliwili ni kitu kinachojulikana wazi wala hakiitaji ufafanuzi zaidi. Hilo ni kwa sababu utumiaji wa maneno kama haya (*terminology*) mara nyingi huzusha mizozo na madhara baina ya wanafalsafa wanazuoni na wana mantiki katika ufafanuzi wa maneno haya.

### Maana ya Roho

Tunaposema roho tunamaanisha au kusudia uhai na nguvu ambazo zinampa mwanadamu uhai na kumfanya aishi. Na nguvu hizi zinapojitenga na kiwiliwili basi uhai wa mwanadamu huwa umeisha hapa duniani.

Hivyo ndivyo tunamaanisha tunaposema roho. Ndipo hapo mbeleni tukatangulia kusema kuwa ni chombo kilichokusanya akili, nafsi na kiwiliwili. Je bila ya roho kuleta uhai kutakuwapo na akili? Na ni kiwiliwili gani kinachoweza kutaharaki bila ya roho? Na nafsi je itaweza kufanya kazi? Na unapoishi muda wa kukaa roho katika kiwiliwili cha mwanadamu basi pia maisha ya mwanadamu huyo huwa yameisha hapa ulimwenguni kisha huenda katika ulimwengu mwengine (Akhera).

**Ni nini Akili?**

Tunaposema akili tunakusudia ile nuru inayomfanya mwanadamu aweze kutofautisha baina ya yale yaliyo sawa na makosa, baina ya ovu na zuri, baina ya liwezekanalo na lisilowezekana. Na kwa maneno mengine ni nguvu zinazomfanya mwanadamu aweze kuzingatia, kupambanua au kufahamu. Na ni kupitia akili ndipo mwanadamu anaweza kuzingatia, kupambanua na kufanya kila jambo.

**Maana ya Nafsi**

Kuhusu kueleza nafsi kumezuka tofauti (ikhtilafu) kubwa baina ya wanafalsafa juu ya kufafanua maelezo yake. Hadi likawapelekea baadhi yao kutoa taarifa (maelezo) zisizopungua arubaini juu ya nafsi.

Lakini tunaposema nafsi tunakusudia sehemu inayomfanya mwanadamu ahisi, apende au achukie kitu au jambo na pia sehemu ya matamanio ya mwandamu. Na Qur'an tukufu mara huita kwa jina hili hili (*Nafsi*) na mara nyingine huiita kwa jina la moyo (*Qalbu*).

**Tofauti ya nafsi na akili**

**a) Akili**

Ni kupitia akili ndipo mwanadamu anaweza kutambua kuwa jambo hili linawezekana na lile haliwezekani. Na kwamba moja ukiongeza moja huwa ni mbili. Na mbili na mbili huwa ni nne. Ni akili pekee ndiyo inayoweza kutambua mambo

haya. Basi elimu, maarifa, kukadiria na hekima vyote hivi vinatokana na akili.

**b) Nafsi**

Ni katika nafsi ndiko kunapatikana hisia za mwanadamu kama vile kupenda na kuchukia. Basi kupenda kwa dhati, ubinafsi, kuwa na khofu na hisia, yote haya yanatokana na nafsi.

Kwa hiyo kuna tofauti iliyowazi baina ya akili na nafsi.

Na kwa maana hii nafsi inatambulika kuwa ndicho kiungo cha hatari zaidi kwa mwanadamu.

Ndio sehemu inayoweza kumfanya aongoke au apotee. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Qur'an Suratush Shamsi: "Naapa kwa nafsi (roho) na aliyeitengeneza, kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa. Na bila shaka amejihasiri aliyeiviza nafsi yake." Basi nafsi ambayo ndiyo sehemu asili ya hisia kupenda au kuchukia. Kwa uwezekano wake mwanadamu huwa mwema, au huenda njia isiyo sawa na kuteleza kwenye uovu, uharibifu na makosa mengine.

**Ni ipi kazi ya akili**

Akili haina kazi ya kuwamrisha kama vile nafsi kwa nini?

Kwa maana akili hutambua mambo na kuyabainisha, kwa mfano inaweza kutambua kwa kufanya kazi na kujihusisha na mazoezi ni vizuri, na kwamba uvivu ni makosa, na pia vile vile kutambua kwamba uadilifu ni jambo zuri na kudhulumu ni uovu, kwa hivyo kazi ya akili katika maisha ya binadamu ni kuweza kutambua mambo na kuyabainisha. Lakini nafsi ndio kama makao makuu, na ndiyo yenye kupanga na kumiliki uendeshaji wa mambo katika makao makuu hayo. Ni chini ya uwezo wa nafsi ndipo unaweza kukubali na kufuata mambo yaliyopitia akilini au kwenda kinyume cha yale mambo

yaliyosemwa na akili. Kwa ajili hiyo ndipo Qur'an tukufu imeeleza juu ya upande huu kwa kusema: "Na wakazikanusha, na hali kuwa ni kweli, lakini walizikanusha tu kwa dhulma na kujivuna" ***(Naml Aya 14).***

Kwa upande huu akili imetoa hukmu na kusema "Hakika ukweli huu ni wa sawa kabisa na umethubutu kisheria na ni wajibu kuufuata" Lakini wao waliupinga pamoja na kuwa na yakini kwamba hayo ni ya kweli .... Unajua ni kwa nini wamepinga? Kwa sababu matamanio yao ya nafsi haya kuwaruhusu kuyafuata maneno au maoni ya akili.

Na katika Aya nyingine Qur'an tukufu inasema: "Na mkaificha kweli ili hali mnajua" ***(Al-Imran Aya 71.).***

Hebu tazameni na mzingatie maneno haya, hakika wao wanajuwa kwamba hii ni haki, kwa maana akili zao zimekiri kwamba jambo hili ni kweli na la haki, akili imetambua usawa na haki ya jambo hili na kumwambia binadamu: Huu ni ukweli lakini matamanio na hisia za nafsi yake ndizo zilizomfanya binadamu afanye kinyume cha yaliyosadikishwa na akili na kisha akaificha haki na kuisitiri isionekane kabisa.

**Vipi akili hutekwa**

Mwanzo akili hutoa rai na kusema: Saumu ni jambo zuri, kwa hivyo ni vyema ufunge, hivi ndivyo akili inavyokwambia. Lakini nafsi huenda isikubaliane na jambo la kufunga na huku hisia zote na matamanio ya nafsi yanakupeleka wewe upande wa kula na kuwacha kufunga. Na pale unapotaka kula unahitaji kutafakari njia bora ya kula, na chakula bora utakachokula, na njia gani unayoweza kupatia chakula. Hapa ni lazima utumie akili yako juu ya mambo haya.

Akili yako hukwambia: "Usile bali funga" lakini ni nafsi yako inakuhimiza juu ya kula, na utakapokubali jambo hilo huwa umetumia akili. Akili hukwambia tena: "sawa, wewe wataka kula badala ya kufunga na mimi sikuungi mkono juu ya kutaka kula."

"Mimi nakwambia funga" kisha nafsi huijibu akili kwa ukali na makemeo "Una nini Ewe akili?" Umetoa maoni yako na kazi yako imekwisha na wala haya hayakuhusu tena, unachotakiwa sasa ni ufanye haraka katika kutafuta chakula na uvumbue njia ya matamanio na starehe."

Basi nafsi hukoma hapo hapo na kusema. "Niko tayari kukutumikia", kisha huitwii nafsi na kuijulisha njia ya kupata mambo hayo.

Mfano mwengine:

Akili husema "Haifai kuiba" kisha nafsi huipinga akili na kusisitiza juu ya kuiba. Lakini kuiba kwataka mipango na ni nani anaeipanga mipango hiyo? Bila shaka ni akili.

Nafsi huiambia akili "Mimi nimeazimia kuiba unalohitajika sasa wewe ni upange mipango ya kuibia", lakini akili haiungi mkono jambo hilo na kujua kwamba wizi si jambo zuri, hapo nafsi huikemea akili na kusema "Wacha upuuzi wako, kazi yako imeisha na mimi sasa nimetilia mkazo juu ya kuiba, unachohitajika ni kupanga mipango ya kuibia. Mwishowe akili huitwii nafsi na huwa ni chombo cha kutumiwa na nafsi katika kutekeleza mambo yake."

Na Imam Ali (a.s.) amesema juu ya uhakika wa jambo hili ya kwamba: "Ni akili ngapi zilizofanywa mateka na kuwamrishwa na matamanio ya nafsi." ***(Nahjul Balagha Hikma Na. 211)***

**Akili ni mateka, lakini kwa nani?**

Akili huwa ni mateka wa matamanio ya mwanadamu. Huiamrisha akili na ikawa iko chini ya amri yake.

Na amesema Imam Ali (a.s.): "Mauti mingi ya akili hutokana na tamaa au matamanio." ***(Nahjul Balagha Hikma Na. 219)***

Na katika maneno mengine ya Imam Ali (a.s.) akieleza kwamba akili hufanya kiasi kipimo chake sawasawa kwa binadamu iwapo haitaongozwa na matamanio ya ulimwengu akasema (a.s.):

“Imeshuhudia jambo hilo akili inapotoka kwenye utumwa wa matamanio na kusalimika kuwa chakula cha ulimwengu.” *(Nahjul Balagha Kitabu Na. 3)*

Na akasema tena (a.s.) juu ya kuchomeka akili kwa ajili ya matamanio: “Hakika akili imeunguzwa au kuteketezwa na matamanio”. ***(Nahjul Balagha Khutba Na. 109)***

Na akasema tena (a.s.): “Matembezi ya akili ni baina ya matamanio na shahawa ya nafsi yake.” ***(Mizanul Hikma Juz. 6 Uk.431)***

Na akasema tena (a.s.): “Adui ya akili ni matamanio” ***(Mizanul Hikma Juz. 6 Uk.436)***

Kwa hiyo nafsi ina uwezo wa kuiamuru na kuipeleka akili namna inavyotaka.

Na hapa unajitokeza umuhimu wa nafsi na hatari inajificha, na Qur'an tukufu inatilia mkazo kwamba kufaulu kwa binadamu ni kutokana na kusalimika kwa nafsi yake. Mwenyezi Mungu (SWT) anasema: “Ama yule aliyegopa kusimamishwa mbele ya Mola wake, akaikatasa nafsi yake na matamanio basi kwa hakika Pepo ndiyo itakayokuwa makazi yake.” ***(An-Naziat 40 41)***

Kwa hiyo mas'ala ni ya nafsi, atakayeitakasa nafsi yake basi amefaulu sana kwa hivyo ni wajibu kwetu kutilia mkazo sana juu ya jambo la kuitakasa nafsi na kuisalimisha kwa Allah (SWT).

**Pengo katika kueleza maana ya mantiki kwa wagiriki**

Wagiriki wameelezea katika kufafanua maana ya mantiki kuwa ni “Chombo cha kikanuni (sheria) kinachoilinda akili kwa kutofanya makosa ya ki mawazo.” ***(Al-Mudhaffar: Almantik Uk. 10)***

Na wakaendelea kueleza juu ya wadhifa na upeo wa mantiki kwamba ni kuepuka makosa na kusahihisha mawazo au fikra kwa mwanadamu.

Na maoni ya mwanachuoni Ibnu Hazmi Al-Andalusy juu ya elimu ya mantiki ni kuwa: "Elimu ya mantiki inavumbua ukweli wa kila jambo na kuweza kulitenganisha kutokana na uongo mpaka kusiwe na shaka kabisa. ***(Dkt Mahdi Fadhlullah Mantik. Uk. 20)***

Lakini elimu ya mantiki ya wagiriki na ile iliyopangwa mipango yake na kugawanyiwa katika sehemu tofauti tofauti na mwanafalsafa Arosto mwaka (322-384 B.C). Je inatekeleza na kufanya wajibu wake ipasavyo?

Jibu ni la hii ni kwa sababu imelemea katika upande wa kutilia umuhimu juu ya umbile la mawazo au fikra. Kwa sababu hiyo ndio ikajulikana mantiki hiyo mantiki ya umbo tupu au kiunzi. Hilo ni kwa sababu mantiki hiyo haikuwa na mipangilio ya uvumbuzi wa chanzo asili cha mambo Fulani (background), na mambo yanayoathiri nafsi na mawazo ya binadamu.

Mwanachuoni Al-Mudarrisi ameeleza kuwa: "Elimu hii ya mantiki inathaminiwa kwa kuwa imepanga mipangilio juu ya muelekeo wa mawazo ya binadamu katika kukabiliana na mizozo na mambo ya kipuuzi yasio na faida. Lakini kwa upande mwengine haikuweza kufanya utafiti juu ya chanzo cha mawazo au fikra. Mfano wa jambo hili ni kama mfano wa yule anaejumlisha tarakimu na kuzigawa bila ya kuzingatia siri au undani wa tarakimu (*numbers*).

Basi mantiki ya Arosto ya umbile tu kwa kule kutilia muhimu wake juu ya umbile la mawazo tu na kusahau kutafiti juu ya undani wa mawazo. Na misingi yake imepelekea kusahau yale yanayoteka nyara mawazo ya binadamu ambayo mwishoe humpotosha: kama vile ilivyosahau wajibu wa akili juu ya kuvipambanua vitu hivi vinavyomteka binadanu mawazo. Kwa hiyo mantiki hii haikuweza kumpa binadamu maendeleo ya ziada katika kupanua mawazo yake."

Kwa hiyo maoni yaliyoenea juu ya elimu ya mantiki,ni kwamba tatizo la binadamu katika ulimwengu ni tatizo la akili. Linaweza kutatuliwa iwapo tu kutawekwa misingi juu

ya utaratibu wa utendaji kazi wa mawazo au fikra. Lakini ukweli ni kwamba, tatizo hili huwa ni la kinafsi kabla halijawa la kiakili.

Hivyo basi iko haja Kwanza ya kupuza tatizo hili katika nafsi kabla hatujaanza kuweka misingi hiyo katika akili na mawazo ya binadamu. Kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu nafsi huathiriwa na matakwa ya binadamu, naye kampeleka kwenye matamanio. Na hapo hubaki ule uwezo wa binadamu juu ya kufikiria au kuzingatia kuwa ni bure na wala huwa haimufai ile misingi iliyowekwa ya kunidhamisha mawazo yake.

**Kutilia umuhumi juu ya nafsi**

Kuna baadhi ya watu ambao wanageuza na kulekeza umuhimu wao katika akili tu na kuipa kipaumbele. Kisha huzijaza akili zao kwa mambo wanayo yaona ni muhimu kuwa na mawazo mbalimbali, wakawa ni mwenye kuzitumikia akili zao kwa ajili ya mambo hayo.

Na vile vile kuna baadhi ya watu wanaoitumikia miili yao sana kwa kuitafutia chakula, vinywaji, starehe na raha. Lakini wengi wao hujaribu kulisahau jambo hili la muhimi ambalo ni kwamba akili na mwili huwa havijawa vyenye thamani iwapo nafsi itakuwa haijakuwa salama. Nafsi hii itakapokuwa na kasoro basi akili kwa njia isiyokuwa sawa amabao hupeleka kuwangamia na kupotea kiwiliwili. Lau tukirudi katika historia na tukatazama kwa makini matukio mbalimbali wakati huu tulionao, tutakuta kwamba kuna baadhi ya watu ambao wanauwezo na ufahamu mkubwa katika elimu na akili, na akili zao zinahifadhi mambo ya muhimu sana. Lakini mbali na haya yote watu hawa huwa wamezama kabisa katika maovu. Na mfano wa karibu zaidi wa watu kama hao ni shetani (Iblisi). Je ule upotofu wake ilikuwa ni kwa sababu elimu yake ilikuwa ni chache? La hasha.

Tatizo la Iblisi halikuwa ni kwa sababu ya uchache wa elimu. Kwani yeye ndiye aliyekuwa mbele na mjuzi sana, anajuwa

mambo tusiyoyajuwa wala hatujayapitia kamwe. Lakini wapi alikosea? Pale aliposema kumjibu Allah (s.w.t.) pindi alipomwambia amsujudie baba yetu Adam: “Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kutokana na moto na akamuumba yeye (Adam) kwa udongo” (**Aa’raaf: 12**) kilichomharibia yeye ni kibri. Na kibri huwa katika nafsi wala si akilini, kwa hiyo hakuweza kufaidika na elimu wala akili yake. Na watu wingi waliopotea na wanaofanya maovu tatizo lao sio ukosefu wa elimu na kujuwa, lakini ni kwa sababu ya maradhi ya kinafsi.

Na amani iwe juu yako ewe Abul Hassan pindi uliposema: “Na yule asiefunza adabu nafsi yake haja nufaika na akili yake.” Na katika maneno mengine ya Imam Ali (a.s.): “Mwenye kujiepusha na matamanio yake basi akili yake iko sawa.” ***(Mizanul hikma Juz. 6 Uk 436)***

Na vile vile anaashiria Imam Ali (a.s.): katika kuwathiriwa akili na maradhi ya nafsi na kutoweza kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Akasema Imam Ali (a.s.): “Tambueni kuwa tamaa huuwa akili ya mtu” ***(Nahjul Balagha Khutba Na. 86)***

“Mtu kujiistaajabia nafsi yake ni hasadi kubwa kwa akili yake.” ***(Nahjul Balagha Hikma Na. 212)***

Na kwa hayo tunapaswa kutilia umuhimu sana upande wa nafsi. Basi nafsi itakapo kuumbwa na maradhi kama vile kibri, majivuno, uoga, uvivu, ubinafsi, chuki na mifano wa hayo. Vyote hivi havifaidishi. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an tukufu: “Nitawaepusha na (kuzingatia) Aya zangu wale wanaotakabari katika nchi.” (***Aa’raf 146).***

Yaani imani hawaafikiani nayo. Basi wale ambao hawakuwaamini Manabii na Mitume ya Mwenyezi Mungu ya, akili zao zilikuwa si sawa na kushindwa kuelewa? La hasha. Bali tatizo lilikuwa limejificha katika nafsi zao kwa kuwa na kibri na kuendeshwa na matamanio.

**Wajibu wetu juu ya nafsi**

Hakika mara nyingi sisi binadamu hutumia wakati mwingi juu ya kuzielimisha akili zetu, na wakati mwengine mwingi tunaupoteza kwa kuupa mwili raha na starehe. Lakini ni wangapi miongoni mwetu wanaotumia wakati wao kwa kuzilinda nafsi zao zisikumbuke na maradhi au kupotoka?

Tukitazama wale watu wanaosoma katika vyuo vikuu vilivyo Mashariki na Magharibi wameelekea katika ujuzi mbalimbali, akili zao ni kubwa. Hakika binadamu hujihisi kuwa ni duni na aliaachwa nyuma mbele ya watu hawa wenye akili kubwa ambazo zimeazimia na kuvumbua njia mbalimbali za mambo ya ufundi wa kileo (*Electronics*). Angaliyeni namna gani zimetua natija inchi za kimagharibi katika kutengeza vyombo mbalimbali na mipango na kuendelea kielimu.

Hii yote ni kazi ya akili iliyo kubwa. Lakini kwa upande wa pili yanachimbuka maradhi ya kinafsi na makosa mbalimbali katika nafsi hizo hizo. Baadaye huzifanya akili na miili hiyo kuwa ni kuni za maovu katika ulimwengu na vile vile kuwa kuni za moto kesho Akhera (Mungu atuepushie mbali).

**Mtazamo wa makosa**

Wakati mwengine binadamu hukosea pindi anapodhani kuwa ule wakati anaoutumia kwa ajili ya kuisalimisha nafsi yake ni kupoteza mda.

Kwa mfano: unapoenda makaburini kwa mazishi ya Muislamu mwenzio unatumia wakati kwa kuenda na kurudi na kule kukaa makaburini. Wakati huu unaweza kusema je ingekuwa nimeutumia kwa kuichangamsha akili kwa kusoma kitabu, au kufikiria juu ya jambo lenye manufaa katika akili yangu, hilo lingekuwa bora. Lakini jambo hili lina faida kwenye akili yangu peke yake. Je napaswa mimi kukosa kuongeza ujuzi na kuitumikia akili yangu? Na nafsi yangu iko katika muelekeo gani? Na iko katika hali gani?

Ninapaswa kuutumia wakati wangu kwa ajili ya kuitakasa nafsi yangu. Na hii ndio siri ya kiislamu ya ibada na siri ya muongozi katika dini. Hakika unapaswa kuutumia wakati wako kwa swala, kumuomba Mwenyezi Mungu, kuhudhuria mazishi na kuipima nafsi yako kama ilivyopokea kutoka kwa Imam al Kadhim (a.s.): asema "Hakuna mtu asiejuwa msimamo wa nafsi yake, kwa sababu anapofanya mema hutaraji malipo mema kwa Mwenyezi Mungu na kushukuru na anapokosa huomba msamaha na Mwenyezi Mungu humsamehe." ***(Mizamil Hikma Juz. 2 Uk. 402)*** Pindi kutakapokuwa hakuna kupima na kulinganisha baina ya kuendelea kwa binadamu kielimu na akili na baina ya usalama wa nafsi yake, basi kutakuwa na hatari kubwa katika maisha ya mbeleni ya binadamu. Kwa hiyo tunapaswa tuzingatie na kutilia mkazo zaidi kutokana na maovu. Na iwe katika utaratibu wetu mipango ya kuilinda hiyo nafsi na maovu.

## MLANGO WA PILI

## HATARI YA NAFSI KATIKA MANTIKI YA KIISLAMU

### Nafsi ni yenye kuamrisha maovu

Daima tabia ya nafsi kutokana na kupenda mambo ya starehe na matamanio humpelekea binadamu kufanya mambo maovu na kukengeuka. Haya ni kwa ajili ya kujistarehesha na matamanio. Na nafsi itakapotawaliwa na matamanio na binadamu akawa hana uwezo na msimamo thabiti wa kuidhibiti nafsi hiyo, basi matamanio hayo humpeleka katika mahali pa maangamivu kwa kuzingatia mustakbali wake kwa upande wa kidunia na Akhera.

Na niliwahi kusoma katika siku hizi hizi habari zilizochapishwa na gazeti (*Al-hayaa*) linalotolewa mjini London. Habari hizi zinatosha kuwa ni ushahidi na mfano mzuri kwa yale yanayomfika mwanadamu katika kurudi nyuma na kutoendelea pindi anapofuata matamanio ya nafsi yake. Gazeti hilo lililotolewa tarehe (27 Januari 1991) (12-7-1411 H) linaeleza yafuatayo:

"Katika mfano wa kuzorota kwa umoja na kupotea kwa tabia (vitu ambavyo vimepotea katika kizazi kipya cha Amerika) ni yale yaliyoshuhudiwa na mahakama ya Washington wiki iliyopita pindi ilipomuhukumu kifungo mama aliyemfungia binti yake mchanga kwenye sanduku la nyuma la gari kwa ajili ya kuingia jumba la starehe la usiku (*Night club*) ili kukutana na rafiki yake wa kiume.

Patricia (mama) mwenye miaka 29, alidai alikuwa ana miyadi na mmoja kati ya marafiki zake katika jumba moja la starehe za usiku. Lakini hakupata mtu wa kumuachia mwanae mchanga (Jane) mwenye umri wa miezi 8 ili amtazame usiku ule. Binti huyu alimzaa na mume wake aliyepita ambaye kwa sababu wameachana tangu miezi mitatu iliyopita. Alieleza alipokuwa amezuiliwa katika makao makuu ya polisi kuwa, "Mimi sifahamu kwa nini mnanidhulumu namna hii! Mimi nilimueka mwanangu katika kigodoro nyuma ya sanduku la

gari na nikamuekea radio ili asikilize nyimbo ili asiwe na khofu kwa ule upweke na ukimya."

Wale waliokuwa wakihakikisha waligundua kwamba bibi huyo alimuacha mwanawe katika sanduku la gari kwa muda wa zaidi ya masaa matatu. Ili dhihiri kwamba mama huyo alikuwa akija kumtazama mwanae kila baada ya nusu saa. Anasema: "Nilikuwa nikimuomba rafiki yangu aniruhusu kwenda haja, kisha huja kumtazama mwanangu Jane. Lakini rafiki yangu alishuku kitu baada ya kuondoka mara kwa mara mwishowe alikataa kuniruhusu kutoka".

Nae John aliyekuwa mfanyikazi wa hoteli moja aliyeleza kuwa aliwahi kupita karibu na gari hilo mara mbili na akasikia mtoto akilia. Lakini haikumjia kuwa sauti ile ilitoka katika sanduku la nyuma ya gari.

Na pia vile vile shahidi mwengine Regina Jackson aliieleza polisi wa Chicago ya kwamba "Mara ya Kwanza nilidhani kuwa kwenye sanduku hilo kuna paka anayetoa sauti hiyo. Kisha nikajongea karibu na kusikiliza kwa makini. Mwisho niligundua kwamba sauti hiyo ilikuwa ni ya mtoto.

Tukapiga simu kwa polisi na wakafika kwa haraka na kulifungua sanduku hilo. Wakampata mtoto amekaribia kuzirai kwa kulia sana na kukosa pumzi. Wakamtwaa mtoto huyo na kulivuta gari hadi kituoni."

Na baada ya muda mchache Patricia (mama mtoto) aliwasili na kumtafuta mwanawe. Akaanza kupiga mayowe kwamba mwanawe ametekwa nyara na gari lake kuibiwa. Lakini mayowe yake hayakuendelea zaidi kwa maana askari walikuwepo karibu wakichunguza na wakamtambua na kumkamata. Walipomueleza ya kwamba wao ndio waliomchukuwa mtoto wake, aliyendelea kupiga mayowe kwa kudai kuwa wao ndiwo waliomuiba mwanawe pamoja na gari lake. Na hakunyamaza hadi alipomsikia mkuu wa askari akimwambia "Umeshtakiwa kwa tuhuma au kosa kumpuuza mtoto wako na kukaribia kumuua."

Hivi ndivyo namna nafsi inavyoamrisha kutenda maovu. Kwa ajili hiyo sheria za dini zimetukataza kuwa na tabia kama hizi zilizotia mizizi kwenye nyoyo na kutulingania katika kujihami na kuwa chunjo kila wakati ili tuwe na msimamo thabiti tunapovutiwa kufanya maovu na kuyapiga vita matamanio ya nafsi.

Qur'an tukufu inaeleza kwa kunukuu maneno ya Nabii Yusuf (a.s.) ambaye ndiye mwenye kupigiwa mfano mzuri kwa kuwa na msimamo thabiti juu ya kujikinga na maovu. Lakini mbali na hayo Nabii Yusuf (a.s.): alikiri na kutilia mkazo ya kwamba nafsi ni yenye kuwamrisha maovu. Na kwamba kumcha Mwenyezi Mungu ndiyo njia pekee ya kuokoka na kuwa na ikhlas, na hiyo ni ishara ya rehma za Mwenyezi Mungu.

1. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kunukuu maneno ya Mtume wake Yusuf (a.s.): "Nami sijatakasika nafsi yangu, kwa hakika (kila nafsi ni yenye kuwamrisha sana maovu isipokuwa ile ambayo Mola wangu ameirehemu" (***Yusuf :53***).

2. Na ameeleza Imam Ali (a.s.) juu ya yale mambo yanayomsibu mwanaadamu pindi anaposahau au kutoijua tabia ya nafsi kwamba ni yenye kuwamrisha maovu. "Hakika nafsi ni yenye kuwamrisha juu ya mambo machafu na maovu mwenye kuiamini humkhini, na mwenye kuitumainia humpoteza, na mwenye kuiridhia humnywesha kinywaji kilicho kiovu kabisa."

3. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Hakika hii nafsi ni yenye kuwamrisha maovu basi mwenye kupuuza humpelekea kwenye kutenda maovu na dhambi."

4. Na nafsi ya mwanadamu inashirikiana na vitimbi na uovu ili kumsoza mwanadamu katika jarife la maovu na yaliyokatazwa. Kwa hiyo inampasa mwanadamu awe na tahadhari na kuwa muangalifu wala asitowe uaminifu wake na kuyaachia uongozi matamanio ya nafsi yake."

Anasema Imam Ali (a.s.): "Hakika nafsi ni yenye vitimbi, ukiamini shetani atakupeleka katika kufanya mambo yaliyokatazwa."

5. Na katika maneno yake Ali (a.s.) aliyomuandikia kiongozi aliyemtawaza yeye misri anasema Imam Ali (a.s.): "Na muamrishe aikhalifu nafsi yake kwa matamanio na kutofuata hawaa ya nafsi yake. Hakika ya nafsi ni yenye kuwamrisha juu ya maovu ila ile iliyoongozwa na Mwenyezi Mungu (s.w.t.)".

6. Nae Imam Zainul-abidina Ali bin Husein (a.s.): amemtanabahisha mwanadamu na kumuonya juu ya tabia ya nafsi yake, kwa njia ya hekima, ameeleza juu ya kuongoka na kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Akasema kwa kunong'ona na Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Mola wangu, kwako wewe ndio nashtaki uamrishaji maovu ya nafsi, na maovu yanayopita, na kukuwasi wewe kuliko kwingi, na kwa hasira zako zilizo wazi, yanayonipelekea mimi kwenye maangamivu, na kunifanya mimi kuwa duni mbele yako, mwingi na kasoro na maovu, nafsi inapokumbwa na shari huwa na wasi wasi, na inapopata kheri huwa inaizuia, imezama katika machezo na upuuzi, imejawa na kughafilika, inanilekeza mimi kwenye upotovu na kunizuia mimi kufanya toba."

7. Na ni wangapi tunaowajua katika historia ambao wamekuwa kama sadaka za nafsi zao zinazowaamrisha maovu na kuwahadaa. Na wale waliouawa katika khawarij kwenye vita vya Nahrawan, akriban watu 4000. Ni mfano mzuri na ulio wazi kwa uhakika wa jambo hili. Mwanzo walikuwa ni katika wafuasi wa Imam Ali (a.s.) lakini wakawa ni wenye kughafilika na kupotea. Shetani aliwahadaa na wakakubali kufuata nafsi zenye kuwamrisha maovu.

Imam Ali (a.s.) alisema pindi alipozipita maiti za Khawarij siku ya vita vya Nahrawan: "Maovu yawe juu yenu, amewadhuru kwa hakika yule aliyewadanganya". Watu wakamuuliza: "Ni nani aliyewadanganya na kuwaghuru ewe kiongozi wa waumini?"

Akawajibu (a.s.): "Ni shetani mpotovu, na nafsi inayoamrisha maovu, na kuwaghuru wao na kuwapa nafasi kubwa ya kutenda maovu, na kuwaahidi ushindi na wakawasokomeza kwa mambo hayo motoni." ***(Nahjul Balagha: Qusarul Hukam Uk. 323)***

## JIHADI KUBWA-JIHADI DHIDI YA NAFSI

Hakika mtihani mkubwa na mgumu Mwenyezi Mungu aliompa mwanadamu katika maisha yake ni mtihani wa nafsi yake mwenyewe. Na msingi wa kufaulu mwanadamu kutokana na mtihani huo yanapatikana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na pia mafanikio ya maisha yake ya mbeleni duniani na Akhera. Kwa ajili hiyo vimekuwa vita dhidi ya nafsi kuwa ni vikubwa na vya hatari vinavyomkabili mwanadamu.

i. Hivyo ni vita visivyoepukika na visivyochagua nani wala nani. Hata Mitume na mawalii pia viliwakabili. Ikiwa mwanadamu anaweza kuvikimbia au kuviepuka vita dhidi ya wengine, lakini vita vya nafsi haviepukiki wala havikimbiliki.

ii. Ni vita vya daima vinavyomkabili mwanadamu maisha yake yote tangu anapokuwa baleghe hadi kufa kwake. Na mwanaadamu anaweza kushinda vita hivi maisha yake yote lakini mwisho wa umri wake hushindwa na vita hivyo dhidi ya nafsi.

iii. Hakika hivyo ni vita vilivyo jumlisha na kuenea katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu katika kila pembe, kifikra au mawazo, kivitendo na maneno, kidalili na ishara au kuwa kimya. Hakika hatari ya maovu na matamanio ya nafsi yanavunja itikadi ya mwanadamu na mawazo yake, hisia zake za muelekeo wa sawa, maneno yake ya kweli na msimamo wake anaoambatana nao.

iv. Na silaha ya kuvunja haya ni kupatikaniwe mafungamano ya nguvu na umoja baina ya mwanadamu na nafsi yake. Kwani nafsi ndicho kitu kilichopo karibu sana na mwanadamu,inaingiliana na kufungamana naye. Na ni ugumu na uzito ulioje kwa mwanadamu kwa kuishi na kuamiliana na adui yake, na akawa yupo karibu nae na kumuamini. Yote haya ndiyo yanayofanya vita dhidi ya nafsi kuwa vya hatari zaidi. Na yamesadikika waziwazi

yale maneno aliyoyasema Mtume (s.a.w.) wa Mwenyezi Mungu (Rehma na amani zimshukie) kwamba jihadi dhidi ya nafsi ndiyo jihadi kubwa kabisa. Na jambo hili limetiliwa mkazo na kuuelezwa kwa upana na maelezo yafuatayo:

1. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) katika Qur'an: "Na ama yule aliyeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake, akaikataza nafsi yake na matamanio (maovu), basi Pepo ndiyo itakayokuwa makazi yake" (*Naziat*). Basi yule mshindi wa vita dhidi ya nafsi yake anastahiki tuzo kubwa nayo ni Pepo. Na hadi mtu kuingia Peponi anastahiki kupitia tabu zote hizi na mashaka.

2. Imepokewa kutoka kwa kiongozi wa waumini Imam Ali (a.s.) akisema: "Mtume (s.a.w.) alipeleka jeshi kwenye vita, na waliporudi aliwaambia "Pongezi kwa watu waliomaliza jihadi ndogo na kubakia kwao wao jihadi kubwa." Akaulizwa: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na ni ipi hiyo Jihadi kubwa?" Mtume (s.a.w.) akasema: "Ni jihadi dhidi ya nafsi," kisha akaendelea kusema "Jihadi bora zaidi ni ile ya mtu kupigana dhidi ya nafsi yake iliyo ndani ya mwili wake." ***(Biharul Anwar cha Majlisi Juz. 70 Uk. 64)*** Na huenda kipande hiki cha mwisho (kilichoelezwa hapo juu) ni ishara au dalili ya kuonesha moja ya hatari ya vita dhidi ya nafsi. Nayo ni mafungamano ya karibu zaidi yaliyopo baina ya nafsi na mwanadamu kama tulivyoeleza hapo mbeleni kwani nafsi ni adui aliye ndani ya mwili wa mwanadamu.

3. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) akisema: "Shujaa siyo yule mwenye nguvu katika vita, bali shujaa na yule anaeweza kuizuia na kuimiliki nafsi yake anapokuwa na hasira." ***(Sahih Bukhari, Adab Hadith Na. 5763)***

4. Imepokewa kutoka kwa Fadhalatu bin Ubaid akisema: "Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.)

akisema: "Mujahid ni yule mwenye kupigana dhidi ya nafsi yake." ***(Sunan Tirmidin, Fadhailul Jihad Hadith Na. 1621)***

5. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Shujaa kati ya watu ni yule mwenye kushinda hawaa ya nafsi yake."

6. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Zitawaleni nafsi zenu kwa kufanya vita vya kuendelea dhidi yake." ***(Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz. 1 Uk. 143)***

7. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Kutengenea kwa nafsi ni kufanya vitu dhidi ya hawaa ya nafsi." ***(Rejea hiyo juu iliyotangulia)***

8. Na akazungumzia Imam Ali (a.s.): juu ya mbinu za vita vya kupambana na nafsi, akasema: "Itakapokusumbua nafsi yako na wewe isumbue basi itakuwa dhalili kwako, na uhadae nafsi yako mwenyewe basi itafuata utakayo wewe." ***(Rejea hiyo juu iliyotangulia)***

   Basi ni juu ya mwanadamu usikubali haraka kushindwa na nafsi wala asidanganyike na vitimbi vya adui. Ni msimamo thabiti wa mwanadamu unaofanya nafsi kuwa duni na dhalili mbele yake. Na ni kule kutahadhari kwake ndiko kunakoishinda ile nafasi ya kumpeleka yeye kwenye maovu.

9. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Ikabili nafsi yako kwa kuipa nyongo na kuipuuza" ***(Ray Shahri: Mizanul Hikma Uk. 144)*** Hilo ni kwa sababu unapoikabili nafsi kwa kufuata matakwa yake inapelekea kuwangamia kwa mwanadamu na nafsi yake pamoja. Lakini ukiikabili kwa kupuuza matakwa yake ndipo kunapatikana usalama wa nafsi.

10. Na amesema tena Imam Ali (a.s.): "Dawa ya nafsi ni kujiepusha na matamanio yake na kutokula utamu wa ulimwengu." ***(Ray Shari: Mizanul Hikma Uk. 144)***

11. Na katika moja za khutba yake anasema Imam Ali (a.s.) kuwa: "Tambueni kuwa hakuna jambo lolote la kumcha

Mwenyezi Mungu ila huwapo machukuzi ndani yake.

Na hakuna jambo lolote la kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ila huwapo matamanio ndani yake. Basi Mwenyezi Mungu amrehemu yule mtu ambaye amejivua kutokana na matamanio ya maovu na akachukia hawaa za nafsi yake. Hakika nafsi sampuli hii ni yenye kuyapinga zaidi maovu yanayolinganiwa na nafsi. ***(Nahjul Balagha Khutba Na. 176)***

Na pia vile vile mujuwe enyi waja wa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ya kuwa Muislamu alalapo na apambaukiwapo nafsi yake huwa haina uwaminifu naye. Na hubakia mtwevu chini ya nafsi.

12. Na katika kumuusia Sharih ibn Haani, Anasema Imam Ali (a.s.): "Mche Mwenyezi Mungu (s.w.t.) usiku na mchana, na ikhofishe nafsi yako juu ya dunia yenye kuhadaa wala usiiamini nafsi yako hata chembe. Na ufahamu ya kuwa usipoizuia nafsi yako kwa mambo uyapendayo kwa ajili ya kuogopa machukivu itakupeleka wewe kwenye kuikanya. Basi kuwa na kuizuia na maovu, na kuwa na uwezo wa kuzimiliki hasira na ghadhabu zako." (***Nahjul Balagha*** Wasiya Na. 56)

13. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Amali bora ni ile isiyopendwa na nafsi yako." (Rejea iliyotangulia juu ***Qusarul Hukam*** Na. 249) Hii ni kwa sababu asli na lengo la kufanya amali ni kuishinda nafsi na kutoifuata."

14. Na anatilia Imam Ali (a.s.): mkazo juu ya kumaliza vita juu ya mwanadamu dhidi ya nafsi. Akasema: "Jueni ya kuwa yule ambaye hatoisaidia nafsi yake mpaka ikawa ni yenye kuzingatia na kuogopa basi hataweza kuifanyia hivyo nafsi nyingine." (***Nahjul Balagha Khutba*** Na. 90)

15. Anasema Imam Ali (a.s.): "Hakika nafsi hii yangu ninaifunza juu ya kumcha Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ili isalimike siku ya khofu kubwa" (Kiyama). (***Nahjul Balagha Khutba*** Na. 90)

Na kama tulivyotangulia kueleza hapo kabla kwamba vita dhidi ya nafsi havichagui nani wala nini. Ikiwa Imam Ali (a.s.) pamoja na utukufu na cheo alicho nacho pia yeye anakumbwa na mtihani huo huo kama viumbe vengine. Na huenda ikawa siri ya kumfanya yeye awe na ubora alio nao ni huku kufaulu kwake katika vita dhidi ya nafsi.

16. Na anasema tena Imam Ali (a.s.): "Kuutumikia mwili ni kuupa vitu unavyovihitaji katika mambo ya starehe, matamanio na kumiliki vitu. Na katika haya yote ni kuangamia kwa nafsi." (***Mizanul Hikma: RayShahri Juz.* 10 Uk 147**)

17. Na kumulika muangaza juu ya tabia ya vita vya nafsi na muelekeo wake anasema Imam Ali (a.s.): "Akili iko pamoja na jeshi la Mwenyezi Mungu, na matamanio (hawaa) ni kiongozi wa jeshi la shetani, na nafsi huwa kati yao na kushangilia, basi yule atakayeshinda, nafsi huingia upande wake." (**Rejea iliyotangulia Juz. 7 Uk. 405**)

Basi akili ndio chanzo cha vita vya baina ya mwanadamu dhidi ya nafsi yake. Elimu na maarifa ndizo silaha kubwa katika kupambana na vita hivi. Na katika kila upande wa wapiganaji ambazo ni akili na matamanio (hawaa) kuna majeshi na silaha. Kwa hivyo haya ni majeshi mawili. Jeshi la Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na jeshi la shetani yanayopambana kwenye uwanja wa nafsi iliopo ndani ya mwili wa mwanadamu.

## NAFSI NA ATHARI ZAKE ZILIZO WAZI KWA MWANAADAMU

Maisha ya mwanadamu ya hapa ulimwenguni na ya kesho Akhera yamekuwa chini ya dhamana ya nafsi yake na yaliyodhalili kwa kuwathiriwa na nafsi. Itakapotakasika nafsi na ikafuata muelekeo wa akili basi mwanadamu huwa amepata uongofu wa hapa duniani na kufaulu kesho Akhera. Na yakiwa kinyume cha hayo kwa kufuata matamanio maovu ya nafsi kwa kukubali mwenyewe mwanadamu, basi maovu na mapotevu hutanda katika maisha yake ya ulimwenguni na ya kesho Akhera.

Na maneno ya muongozo wa kidini yametilia mkazo juu ya ukweli wa jambo hilo kama ifuatavyo:

1. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Na naapa kwa nafsi na aliyeitengeneza. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake) na bila shaka amejihasiri aliyeiviza." (***Suratu Shams 7-10***). Basi kufaulu na kutengeneza kunatokamana na kutakasika kwa nafsi yake. Na maangamivu na kutofaulu kunatokamana na kuifauata njia ya upotovu ya nafsi. Na kama vile nafsi inapokea utakaso kupitia uchaji Mungu, basi nayo imejiandaa kwa kuenda kombo na kutenda maovu.

2. Anasema Imam Ali (a.s.): "Asilaumu mwenye kulaumu ailaumu nafsi yake. (***Nahjul Balagha Khutba*** Na. 16) Nafsi ndiyo ambayo inatengeza mustakbali wa mwanadamu. Na anapoitambua njia ya sawa ya mustakbali wake basi hakuna anaebeba wajibu huo isipokuwa ni nafsi yake mwenyewe."

## MIONGONI MWA MARADHI YA NAFSI

Maovu na matatizo yanachimbuka kutokana na ile hali ya maradhi ambayo yanatokana na nafsi na kumea na kukulia ndani yake. Basi ni ipi hiyo hali ya kuwa na maradhi? Na vipi atayatibu mwanadamu?

Haya ndiyo yatakayozungumziwa na baadhi ya dalili kutoka katika Qur'an na dini kwa jumla. Na ni hizo zifuatazo:

1. Kuweza mwanadamu kumvua ndugu yake na kumpokonya haki yake katika maisha inachukuliwa kuwa dhambi kubwa mno. Na mwanadamu anapofanya kosa hili huwa ni matokeo ya hali ya kuwa na maradhi katika nafsi. Na Qur'an tukufu inazungumzia juu ya kosa la Kwanza la kuuwa lililotokea hapa ulimwenguni pale Qabil mtoto wa Adam alipomuua nduguye Habil. Na Qur'an imelihesabu kosa hili kuwa linatokana na nafsi.
   Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Basi nafsi kumuuwa nduguye; akamuuwa na akawa ni miongoni mwa wenye kuhasirika." (***Suratul- Maida*** Aya 30).
2. Na khofu au kicho hutokana na nafsi. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Basi Musa akaona khofu katika nafsi yake. Tukasema "usiogope!
   Hakika wewe ndiye utakayekuwa mwenye kushinda." (***Suratut-Taha Aya 68***).

3. Na ubakhili pia ni katika maradhi ya nafsi.

   Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) "Mcheni Mwenyezi Mungu mwezavyo. Na sikilizeni (mnayoambiwa) na tiini na toeni (katika njia za kheri) itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na wenye kuepushwa na ubakhili wa nafsi zao, hao ndio wenye kufaulu." (***Suratut-Taghabun Aya 16***).

4. Na nafsi ndiyo inayompambia mwanadamu mambo maovu na kumpeleka yeye kukengeuka mambo ya dini na sheria zake. Kama ilivyotokea wale Samiry rafiki yake Nabii Musa (a.s.) alipowapoteza wale waliokuwa

wameamini kwa kuwaongoza juu ya kuwabudu ndama wa sanamu aliyemtengeza kwa mapambo ya dhahabu.

Mwenyezi Mungu anasema (katika ***Suratut- Taha Aya 96***) Akasema: "Niliona wasiyoyaona na nikashika sehemu chache ya mwendo wa Mtume. Kisha nikautupa: Na hivi ndivyo ilivyonielekeza nafsi yangu."

5. Na matamanio maovu ya nafsi ndiyo sababu iliyowafanya Mitume kupingwa na kufanyiwa uadui.

Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) katika ***Suratul-Baqara*** **Aya 87:** "Kila walipowafikieni Mitume kwa yale yasiyoyapenda nafsi zenu mlijivuna, kundi moja mkalikadhibisha na kundi (jengine) mkaliua."

6. Na nduguze Nabii Yusuf (a.s.): walisimama dhidi yake kumetendea uovu ule pindi walipomtupa kwenye kisima.

Yusuf (a.s.) alikuwa alikuwa na uzuri wa pekee. Hakika walitenda hilo kwa ajili ya upotevu wa nafsi uliowakumba.

Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an (***Surat Yusuf Aya 18***) kupitia maneno ya baba yao Yakub (a.s.): "Akasema (baba yao) Bali nafsi zenu zimekupambieni jambo (la kumdhuru mwenzenu) basi (langu mimi) ni subra njema; na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayoyasema."

7. Na husda pia ni miongoni mwa maradhi ya nafsi baina ya mtu na jamii kwa jumla. Anasema Mwenyezi Mungu ***(katika Suratul- Baqarah Aya 109):*** "Wengi miongoni mwa watu waliopewa Kitabu wanapenda wangekurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuwamini kwenu, kwa sababu ya husda iliyomo nyoyoni mwao."

8. Na kibri ni maradhi yaliyojenga kiota ndani ya nafsi. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) katika (***Suratul-Furqan Aya 21)*** "Bila shaka wamejitukuza katika nafsi

zao na wameasi uasi mkubwa."

9. Na kuipa nyongo na kujitenga na dini na ujumbe ulioletwa na Mitume ni hali ya kukengeka kwa nafsi, Qur'an imekieleza kitendo hicho kama "upumbavu."

   Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) katika (***Suratul-Baqara Aya 130)***: "Na ni nani atajitenga na mila ya Ibrahim (akaichukia dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu."

10. Anasema Imam Ali (a.s.): "Maafa ya nafsi ni kuilekeza na kuitawaza mambo ya kilimwengu." (***Mizanul Hikma: Rayshari Juz.*** 10 Uk 147)

11. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Mtu kujistajabia nafsi yake ni hasadi kubwa kwa akili yake. (***Nahjul Balagha: Qusarul Hukam*** Na. 212)

## KWANZA NI KUREKEBISHA NAFSI IWE KATIKA NJIAYASAWA

Jambo la mwanzo na la muhimu analopaswa mwanadamu kulifanya na kulitilia mkazo ni kuirekebisha nafsi yake. Kwa sababu jambo hilo ndio ufunguo wa kuongoka kwake. Na pia kwa ajili hiyo ataweza kuyatibu matatizo yote yanayomkabili na kupata mambo mbalimbali ya kimaisha. Na atapata faida kubwa na kupata uongozi ulio sawa kwa uwezo atakaopewa na Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Ama kwa ajili ya kukengeuka nafsi mambo yote anayoyachuma mwanadamu na mali anayoipata hapa duniani huenda yakampelekea kwenye mwisho mbaya. Na ikawa ni njia ya kumpeleka kwenye maangamivu pamoja na wengine na kupatwa na madhara.

Elimu, mali, nguvu, uzuri au uwezo wowote wa mwanadamu yatakapoendeshwa na nafsi iliyopotea, kwa kufuata matamanio mabaya, huenda ikasababisha harasa, maovu na uvunjifu kwa mwanadamu mwenyewe na kwa wengine.

Na majanga yanayomfika mwanadamu wa leo na aliyepita yanatosha kuwa ni rekodi kubwa ya ushahidi na dalili ya ukweli na iliyo wazi juu ya jambo hili.

Kwa ajili hiyo yamekuwa maelezo ya kidini ni yenye tabia ya kutilia umuhimu juu ya kurekebisha nafsi na kujirekebisha mwanadamu katika maisha. Kama tutakavyoona kwenye ushahidi ufuatao. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

1. "Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyomo kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao" ***(Raad: 11).***

2. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Yule asiyeifunza nafsi yake kutenda mema, haja nufaika na akili yake". (***Mizanul Hikma: RayShahri Juz.*** 10 Uk. 145) Na kama ilivyotangulia katika mlango wa Kwanza katika kitabu hiki ya kwamba akili hutoa rai yake na msimamo wake katika kufuata jambo, lakini nafsi kwa kufuata matamanio yake maovu huizima sauti ya akili na kumpelekea mwanadamu katika kuikhalifu.

3. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Aliyeshindwa miongoni mwa watu ni yule aliyeshindwa kuirekebisha nafsi yake" (*Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz.* 10 Uk. 146)

   Basi yule atakayeshindwa kuirekebisha nafsi yake atawezaje kuzirekebisha nafsi za wenziwe na mambo ya maisha.

4. Na akasema Imam Ali (a.s.): "Aliyeshindwa miongoni mwa watu ni yule anayeweza kuondoa ila katika nafsi yake na asifanye." (*Mizanul Hikma: RayShahri Juz.* 10 Uk. 146)

   Na mwanzo mwanadamu huwa anauwezo wa kuondoa ila katika nafsi yake lakini matamanio ya nafsi yake ndiyo yanayomzuia. Na mwenye kushindwa kuyazuia matamanio maovu ya nafsi yake basi hatarajiwi kunusurika katika maisha.

5. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Mwenye kuirekebisha nafsi yake huimiliki. Na mwenye kuiacha nafsi yake (juu ya matamanio maovu) humuangamiza." (*Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz.* 10 Uk. 146)

6. Na maisha yana thamani gani yawapo chini ya utumwa na mateka ya matamanio maovu? Na huwa ni jahima wa maasia na makosa, na huwa ni makazi ya ufisadi na shari.

   Anasema Imam Ali (a.s.): "Asiyedhamini kuondoa kasoro katika nafsi yake hushindwa na matamanio maovu. Na aliye kwenye kasoro basi ni bora afe." (*Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz.* 10 Uk. 146)

7. Na jambo baya zaidi ni pale atakapohisi mwanadamu kwamba amejitosheleza kwa nafsi yake juu ya kuirekebisha na kuona kuwa hana haja ya kifunza muongozo mwema. Hapo Mola humkasirikia na watu kumchukia kwa kuzama katika upotovu na ufisadi. Anasema Imam Ali (a.s.): "Mwenye kuiridhia nafsi yake huzidi wa kumkasirikia." (*Nahjul Balagha, Qusarul Hukam* Na. 6)

8. "Enyi watu! Kuweni ni wenye kuzifunza nafsi zenu na zirekebisheni kipumbavu." (***Nahjul Balagha, Qusarul Hukam*** Na. 359) Haifai kufuata mazoea ya jambo ambalo halikuwamrishwa na dini ya kiislamu ambalo halikuswihi sheria ikiwa ndani yake kuna uovu. Na hapaswi mwanadamu kufuata mazoea mabaya ya nafsi yake hata kama imejimakini vipi katika maisha.

9. Na Imam Ali (a.s.) aliandika kumuusia mwanawe Imam Hasan (a.s.): katika baadhi ya mambo aliyomuusia ni "Na nimeona kuhusika kwangu mambo ni jambo lenye kumhusisha mzazi mwenye mapenzi. Na nimekusanya ndani yake mambo ya adabu kwako. Na iwe hivyo mpaka umri wako na huku ukikaribia kuiacha dunia (kuwa mzee). Hali ya kuwa ni mwenye nia ya sawa na nafsi iliyo safi." (***Nahjul Balagha,*** Kitabu Na. 6)

   Katika mwanzo wa maisha na kabla nafsi haijajisonga katika maslaha na mambo mengine yakilimwengu, huwa kuirekebisha ni rahisi na bora zaidi.

10. Imepokewa kwa Imam Ali (a.s.): kuwa "Hakuna aliye bora kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) hapa ulimwenguni kama nafsi inayofuata na kutwii maamrisho yake (s.w.t.)." (***Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz.* 10 Uk. 125**)

11. Na kutoka kwake Imam Ali (a.s.): "Sababu ya kuongoka nafsi ni kumcha Mola (s.w.t.)." (***Mizanul Hikma:* Uk. 144)**

12. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Mwenye kuikemea nafsi yake na kuikosoa huwa ameiongoza. Na mwenye kuisifu huwa ameichinja na kuiua." (***Mizanul Hikma* Uk. 144)**

13. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Mwenye kujiepusha na matamanio maovu akili yake huwa iko salama na nzima." (***Mizanul Hikma Juz.* 6 Uk. 432**)

14. Na katika maneno mengine ya Imam Ali (a.s.): akiashiria kuwa akili haifanyi jukumu lake kikamilifu katika maisha ya mwanadamu mpaka itakapoathiriwa na matamanio maovu ya nafsi. Akasema (a.s.): "Akili uhakikisha na kushuhudia jambo hilo inaposalimika kutoka kwa mateka ya matamanio ya nafsi na kuepuka kuwa chakula cha ulimwengu na mafungamano yake." (***Nahjul Balagha Kitabu:*** 3)

## NAFSI NI ADUI ALIYE HATARI ZAIDI

Mwanadamu kumjua adui yake na kugundua mbinu zake za kivita, humfanya aweze kumkabili kwa urahisi na kumshinda. Na kila anapojificha adui na kufichika mbinu zake za kivita huwa kupambana naye ni hatari na vigumu.

Hapa ndipo linapojificha lile tatizo lililopo baina ya mwanadamu na nafsi yake. Kwa maana ya uadui wake haujitokezi kiurahisi. Kama vile ilivyo na ujuzi mbalimbali wa kutumia vitimbi vya kuhadaa ambavyo mwanadamu asiweza kuvitambua kabisa, au asiweze kuhisi athari ya ule uadui.

Na umuhimu wa maelezo ya kidini na muelekeo wake yanazungumzia kwa kina juu ya mwanadamu kuielewa nafsi yake, na kuweka wazi mambo yanayoyataka nafsi, ili awe na tahadhari anapoamiliana nayo.

1. Mtume (s.a.w.) amesema: "Anayemsaidia adui yako ni nafsi yako iliyo ndani ya mwili wako." (***Biharul Anwar: Majlisi Juz.* 70 Uk 64**)

2. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Adui ya akili ni matamanio maovu ya nafsi." (***Mizanul Hikma: RayShari* Juz. 6 Uk 336)**

## KUIHESABU NAFSI NA KUICHUNGA

Kuwepo kwa tabia ya kupenda machafu na kulemea kwenye matamanio katika nafsi ya mwanadamu ni jambo lisilobudi kwake. Hiyo ni hikma yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Lakini kuziongoza tabia hizi za kupenda machafu ndio wajibu wa mwanadamu alioumbwa kwa ajili ya hayo.

Na ni juu ya mwanadamu kupambanua kwa akili yake njia bora ya kuivua nafsi na maovu haya, na kuzingatia kwa makini mambo yanayopendwa na nafsi ili azuiye kukuwa kwa ufisadi. Na aweze kuyaponya maradhi ya hatari ya nafsi. Na aweze kuweka mpaka kwa yale yanayoweza kutatokea katika makosa.

Kama vile mwili unavyohitaji kuoshwa na kusafishwa na mambo mengine ya kawaida, na kupozwa kutokana na maradhi. Hivyo hivyo nafsi inahitaji kushuhulikiwa kila wakati na kuchungwa daima ili kuihifadhi na madoa na uchafu.

Na yanakuja maelezo ya kidini kwa umbo la wazi kueleza dharura ya kutegemea muelekeo thabiti na mbinu za kudumu katika kuihesabu nafsi na kuichunga.

1. Mtume (s.a.w.) amesema: "Mwenye akili anapaswa kugawanya masaa, wakati wa kumuomba Mola wake, wakati mwengine wa kuihesabu nafsi yake, na wakati mwengine wa kufikiri yale aliyotendewa na Mwenyezi Mungu (s.w.t.)." ***(Biharul Anwar: Majlisi Juz.* 70 Uk 64)**

2. Na kutoka kwa Mtume (s.a.w.) amesema: "Mja hajawa mumini wa kweli mpaka aihesabu nafsi yake na kama bwana anavyomhesabu mtumwa wake." ***(Biharul Anwar: Majlisi Juz.* 70 Uk 64)**

3. Na kutoka kwa Ima Jaffar Sadiq (a.s.) amesema: "Basi zihesabuni nafsi zenu kabla hazijahesabiwa, kwani siku

ya Kiyama kuna sehemu hamsini, kila sehemu watu watasimamishwa miaka elfu moja kisha akaisoma Aya hii: "Siku ambayo muda wake ni miaka elfu hamsini" ***(Maarij 4).*** (***BiharulAnwar: Majlisi Juz.*** **70 Uk 64**)

4. Na kutoka kwa Imam Musa al-Kadhim (a.s.): akisema: "Hakuna mmoja wetu ambaye haihesabu nafsi yake kila siku akifanya mema hutaka kufanya zaidi, na humshukuru Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Na akitenda maovu hutaka msamaha kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na kutubia." (***BiharulAnwar: Majlisi Juz.*** **70 Uk 64**)

5. Na anatahadharisha Imam Ali (a.s.): juu ya kutowajibika kuihesabu nafsi na kuichunga. Akasema "Mwenye kuiachilia nafsi yake basi amejipoteza." (***Mizanul Hikma: RayShahri: Juz.*** **10 Uk. 146**)

6. Imepokewa kutoka kwa Shaddad bin Aus kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Mwerevu ni yule mwenye kuihesabu nafsi yake na kufanya yatakayomsaidia baada ya kufa. Na dhaifu ni yule afuataye matamanio maovu ya nafsi yake na akataraji mema kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.)." Akasema kuwa Hadith hii ni *"Hasan."*

   Akasema kufafanua maana ya kuihesabu nafsi ni kuwa akaihesabu nafsi yake hapa hapa ulimwenguni kabla ya kuhesabiwa siku ya Kiyama.

   Na imepokewa kutoka kwa Umar bin Khattwab akisema "Zihesabuni nafsi zenu kabla hazijahesabiwa, na muzipambe kwa ajili ya siku kubwa (Kiyama). Hakika hesabu itakuwa rahisi siku ya Kiyama kwa yule aliyeihesabu nafsi yake hapa ulimwengu.

   Na imepokewa kwa Maimun kutoka kwa Mahran akisema: "Hajawa mja mchaji Mungu wa kweli mpaka aihesabu nafsi yake kama anavyomuhesabu mshirika wake kula chakula chake na mavazi yake yanatoka wapi?"

7. Na ni juu ya mwanadamu awe madhubuti juu ya kuihesabu

nafsi yake na kuichunga. Anasema Imam Ali (a.s.): "Mwenye kuizuia nafsi kwa yale anayoyapenda, humtaabisha yeye kwa yale anayoyachukia." (***Mizanul Hikma: Ray Shhari Juz.* 10 Uk 146)**

8. Na akasema Imam Ali (a.s.): "Mwenye kuihesabu nafsi yake amefaulu, na mwenye kuisahau amengia kwenye hasara." (***Nahjul Balagha Qusarul Hukam Hikma* Na. 208)**

9. Na akasema tena Imam Ali (a.s.): "Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, zipimeni nafsi zenu kabla hazijapimwa, na mzihesabu kabla hamjahesabiwa." (***Nahjul Balagha Khutba*** Na. 90)

   Na hivi ndivyo yanavyotilia mkazo maongozi ya dini juu ya ulinganishaji kujihesabu mwanadamu nafsi yake katika ulimwengu na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kuihesabu kesho Akhera. Kila atakapo dumu mwanadamu katika kuingoza na kuichunga nafsi yake duniani, huipunguzia nafsi yake shida ya hesabu siku ya Akhera. Ama kuupuza kwake na kujisahaulisha katika kuihesabu nafsi yake hapa duniani, jambo hilo litamtia yeye kwenye mashaka na adhabu mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) wakati wa hesabu Akhera.

10. Ajabu iliyoje kwa mwanadamu anasahau kuihesabu na kuichunga nafsi yake na kutazama makosa yanayofanywa na wengine. Na kuzungumza aibu na makosa yao. Anasema Imam Ali (a.s.): "Ihesabu nafsi yako mwenyewe kwa mwenyewe, kwani nafsi nyingine zina wenyewe wa kuzihesabu." (***Nahjul Balagha Khutba* Na. 222)**

## NATIJA YA KUPOTOKA KWA NAFSI

Hakika matatizo na hatari yanakumba nafsi katika upotovu na maradhi, ni matatizo na hatari kubwa sana. Yametanda katika kila upande wa maisha ya mwanadamu, na kujaza matukio yake yakilimwengu na Akhera kwa hasara na maovu. Na mtu ambaye atakuwa ana mori na dhati yakuondoa hatari hizi na kujiepusha na madhara, vipi mtu huo ataweza kufurahia matatizo haya na hatari hii iliyokubwa? Na vipi ataweza kuiridhia nafsi yake kuwa kwenye maangamivu na machafu kwa ajili ya matamanio machache na mapato dhaifu?

Hakika iko haja kubwa kwa mwanadamu huyu ya kukumbushwa, kuongozwa na kupewa mawaidha ili asije akateleza katika shimo hili la hatari. Na hilo ndilo lengo la maelezo ya dini yafuatayo:

Na kwa ukweli unaokubaliwa na wote Qur'an inaegemeza mambo yote yanayomsibu mwanadamu kuwa ni kutokana na nafsi yake. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema: "Na ubaya uliokufika unatoka nafsini mwako." ***(Nisaa 79).***

Na katika mujtamaa au kwa watu binafsi chanzo cha kutoendelea na kushindwa mwanadamu kinatokana na hali ya nafsi.

Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) "Ulipokufikieni msiba ambao nyinyi mmekwisha watia (maadui) mara mbili ya huo mnasema: "Umetoka wapi huu? Sema: "Huo umetoka kwenu wenyewe." Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye uweza juu ya kila kitu." ***(Aali Imran 165).***

Na Aya tukufu inazungumzia juu ya kushindwa kivita ambako kuliwapata Waislamu katika vita vya uhud. Hilo lilitokana na hali mbaya ya nafsi ilizozikumba nyoyo za wapiganaji, hasa wale warushaji mishale vilivyokuwa kileleni mwa mlima. Wakaondoka mahali hapo kwa ajili ya kufuata ngawira.

Jambo ambalo liliwawezesha maadui zao kuzingira mahali hapo na kushinda vita. Kama vile ilivyo maarufu katika historia.

3. Na anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) "Hayo (ya kuwafuka balaa hizi) ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, hata wabadilisha wao yaliyomo nyoyoni mwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (kila jambo) na ni Mwenye kulijua." ***(Al-Anfal 53).***

4. Imepokewa na Anas kutoka kwa Mtume (s.a.w.) kuwa amesema: "Pepo imezingirwa na mambo ya machukizi, na moto umezingirwa na matamanio maovu." (***Sahih Muslim Kitabu cha Al-janna*** **Hadith Na. 2823)**

5. Na anasema Imam Ali (a.s.): "Usiiruhusu nafsi yako kuyafuata matamanio, na kufadhilisha starehe za ulimwengu, jambo hilo litaharibu dini yako wala haitotengenea, na itaitia nafsi yako hasarani wala haitopata faida." Hakika hiyo ni hasara ya ulimwenguni na kesho Akhera. (***Mizanul Hikma: Ray Shari Juz*** 10 Uk 431)

6. Hakika katika madhara makubwa ya kukengeuka kwa nafsi ni kuiathiri akili. Inapooza uwezo wake na kuvunja kazi yake. Anasema Imam Ali (a.s.): "Matembezi ya akili ni baina ya hawaa na matamanio maovu." (***Mizanul Hikma: Ray Shahri Juz*** 6 Uk 431)

Na kunabaki nini kwa mwanadamu inapoondoka akili yake? Na nini thamani yake baada ya hilo?

7. Na anatahadharisha Imam Ali (a.s.): juu ya kusalitiwa akili na matamanio ili akili iwe ni chombo chake (matamanio) cha kukipoteza, badala ya kufanya mambo ya muongozo na muelekeo mwema. Akasema (a.s.): "Matamanio maovu yameichoma akili yake (ya mwanadamu). (***Nahjul Balagha Khulba*** **Na. 109)**

8. Na Imam Ali (a.s.): alimuandikia Muawiya bin Abi Sufyan akisema: "Hakika nafsi yako imekutia kwenye shari, na kukupeleka kwenye dhambi, na imekunywesha maangamivu na kukusahilishia wewe njia ya kuenda kwenye maovu." (***Nahjul Balagha Khulba*** **Na. 30**)

## MLANGO WA TATU

## HATARI YA KUANGUKA KWENYE MAOVU

Kwa nini tunarudia mara kwa mara katika Swala zetu kila siku kwa kusema "Tuongoze njia iliyonyooka." Kwani sisi hatujihesabu kwamba ni Waislamu tulioamini tunaofuata njia iliyonyooka? Je tuna shaka na njia hii tunayoifuata na kuzidhania nafsi zetu kuwa zimepotea? Au ni vipi?

Ukweli ni kwamba njia hii iliyonyooka sio njia anayoitafuta mwanaadamu pahali palipo na njia nyingi tafauti tafauti. Kisha atakapoipata njia hiyo aendelee nayo kwa mara moja mpaka mwisho. Bali mwanadamu kila wakati anapokabiliana na tukio, jambo au neon hukuta mbele yake njia nyingi moja tu ndiyo iliyonyooka lakini zilizobaki zote zimeenda kombo.

Na kila wakati mwanadamu anajitokeza wazi katika hatari ya kukengeuka na kwenda kombo na njia iliyosawa ambayo anaifuata, kwa ajili hiyo ndio anarudia mara kwa mara anaposali kwa kusema, "Tuongoze njia iliyonyooka." Kinachotakiwa sio kutambua njia ya sawa na kuwanza kuifuata katika maisha. Bali kinachotakiwa ni kuwa na msimamo wa kuendelea kuifuata njia hiyo.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anatuelekeza tutake kinga na salama kutoka kwake kutokana na maovu na kupotea baada ya kutuongoza. Basi tunapaswa kusema "Mola wetu usizipotoe nyoyo zetu baada ya kutuongoza na utupe rehema itokayo kwako, hakika wewe ndiwe mpaji mkuu." ***(Aali-Imran 8).***

Na katika mapokezi mengine anatukumbusha Mola (s.w.t.) kisa cha yule mwanadamu mkubwa wa mayahudi Bal'am bin Bara kama mfano mbaya wa kuwangukia katika hali za kikafiri na upotevu, baada ya kuwa ameshikamana na uongofu. Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t.) "Na wasomee habari za wale tuliowapa Aya zetu (kuzijua) kisha wakajivua nazo (wasizifuate) Na shetani akawaandama, wakawa miongoni mwa waliopotea. Na kama tungelitaka

tungeliwanyanyua kwanzo, lakini wao waligandamana na ardhi na wakayafuata matamanio yao. Basi hali yao ni kama hali ya mbwa; ukimpigia kelele (hukimbia na huku) anahema, na ukimwacha pia huhema. Hiyo ndiyo hali ya watu waliozikadhibisha Aya zetu. Basi simulia Hadith huenda wakatafakari."

Na hakuwa Iblisi ni mwenye kumuabudu sana Mwenyezi Mungu na kunyenyekea hadi Mwenyezi Mungu akampandisha kwenye cheo cha Malaika pamoja na kuwa yeye alikuwa ni katika majini. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Isipokuwa Iblisi ambaye alikuwa ni miongoni mwa majini." Lakini kwa kosa lake hilo mara moja amekuwa ni mfano wa maovu na upotovu hadi siku ya Kiyama. "Na alikuwa amemuabudu Mwenyezi Mungu (s.w.t.) miaka elfu sita, haijulikaniwi ni miaka ya ulimwenguni au duniani." (***Nahjul Balagha Khutba*** **Na. 192**) Kama alivyosema Imam Ali (a.s.)

Na yanatueleza mapokezi juu ya baadhi ya mifano ya kihistoria iliyokumba na utelezi na kuwangukia kwenye maovu baada ya kutumia muda mwingi katika mwenendo wa uongofu. Kama mfano wa Barsisa, yule mchaji Mungu mkubwa ambaye alikuwa ni kigezo chema katika kucha Mungu na kunyenyekea katika jamii moja ya mayahudi. Na cheo chake kwa Mwenyezi Mungu alikuwa ni mwenye kutakabaliwa maombi yake. Akiletewa wenda wazimu na wagonjwa akiwaombea na kuwatibu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Na siku moja aliletewa mwanamke mzuri na mwenye utukufu aliyeshikwa na maradhi ya wazimu. Ndugu zake wakamwachia Barsisa ili amtibu kwa baraka alizokuwa nazo.
Mara mchaji Mungu yule kwa ghafla anatenda tendo chafu na yule mwanamke mwenye wazimu aliyeletewa amtibu. Na baada ya kufanya tendo hilo la uchafu ndiyo ikamjia akilini mwake kuwa huenda mwanamke huyo amebeba mimba yake.

Ni fedheha iliyoje na aibu hii..... Basi akaamua amuuwe na kumzika jangwani ili asikumbwe na fedheha hii. Lakini fedheha ile ilikuwa wazi na yeye kujulikana. Ikamlazimu akubali mbele ya uongozi na akahukumiwa kifo kwa kusulubiwa baada ya kudhihiri makosa mawili makubwa: kuzini na kuuwa.

Shetani akamwendea huku amesulubiwa akisubiri mauti akapumzika na maisha ya aibu. Shetani akamshawishi kwa kumwambia: "Mimi ndimi niliyekupelekea kwenye jambo hili basi nisujudie mara moja tu ili nikuokowe." Akasema yule bwana kumkubalia shetani "Nitakusujudia vipi na mimi niko katika hali hii?" Shaitan akamjibu "Ishara ya kichwa tu inanitosha."

Basi yule bwana akamsujudia shetani kwa ishara ya kuinamisha kichwa chake.... Na baada ya hilo tu alivuta pumzi zake za mwisho na kuaga dunia. (***Safinatul Bihar Juz*. 1 Uk. 71)**

Hakika yameisha maisha yake huku mikono yake imejaa madoa ya maovu mabaya. Kosa la uzinifu, kisha la kuua kisha akamkufuru Mwenyezi Mungu (S.W.T..) na kumsujudia shetani baada ya kuwa mchaji Mungu mwenye kukubaliwa dua zake mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.).

Hivi ndivyo inavyokuwa kwa mwanaadamu namna itakavyokuwa mwenye imani hukumbani na hatari ya kuwanguka kwenye maovu na kwenda kombo wakati wowote maishani mwake.

Anasema Mtume (s.a.w.) "Muumini haachi kuhofia mwisho mbaya wa maisha yake, asiwe na hakika ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu mpaka wakati anapoaga dunia."

Kuna maelezo mingi ya ushahidi wa kidini na Hadith zenye kueleza kuwa muumini hakabiliwi na hatari upotevu na kukengeuka kama watu wengine, bali hali hii kwake yeye huwa ya hatari zaidi kwa kukabiliwa na mambo haya. (***Safinatul Bihar Juz*. 2 Uk. 209)**

Siku moja aliulizwa Imam mmoja (a.s.) na baadhi ya wanafunzi wake "Ewe kijana cha Mtume watuhofia sisi kutokana na shetani? Imam akajibu: "Khofu yangu juu ya shetani ni kwenu nyinyi (wachaji Mungu) tu, ama wengine wasio nyinyi ashafanya kazi yake kwao."

## HATARI INATOKEA WAPI?

Lakini ni kwa nini mambo ya kumfanya mwanaadamu akengeuke iko sana mbele ya maisha ya muumini?

Inaonekana kuwa kuna sababu nyuma yake hasa kwa sisi tulioamini katika zama hizi.

**Mosi: Kufeli katika malezi**

Wazazi wetu, walezi wetu na malezi tuliyokulia nayo haya kuwa kwa namna inavyoakiwa na mafungamano ya Uislamu. Hakika wengi katika walezi katika jamii yetu hawajui chochote katika mambo ya ulezi wala mienendo ya Kiislamu katika malezi na miongozo ya watoto. Hakika utamaduni wanaoufuata watu wetu na kuupalilia kwenye fikra zetu si utamaduni ulio safi. Lakini imechanganyika na maovu na mambo yasiyo na muelekeo wa kidini. Na tabia na njia za kuwamiliana ambazo tunakulia chini yake haziambatani na yale yanayotaka Uislamu mia kwa mia bali zimejawa na makosa na upotovu.

Hivyo basi anakulia mwanaadamu katika hali hii. Hata nafsi yake ikikubali kutengenea na akafuata njia iliyonyooka chembe chembe za malezi yale huenda zikabakia katika nafsi yake ili zimsoze kwenye upotovu.

**Pili: Shinikizo dhidi ya mafungamano ya kidini**

Katika ulimwengu huu wetu wa sasa wakupenda anasa tunaoishi ndani yake imekuwa kule kujitolea kwa ajili ya anasa ndio msingi na chanzo cha mazito yote haya na matatizo na dhiki katika maisha ya muumin.

Na amesema kweli Mtume wetu (s.a.w.), Pindi aliposema: "Utawajia watu wakati itakuwa mwenye kushika dini ni kama mwenye kushika kaa la moto."

Msukumo huu na dhiki hizi ambazo zinamsumbua mwanaadamu aliyeamini zinazotoka kwa madhalimu na waharibifu wa jamii na hata kutoka kwa jamii na walezi wao

na kupambana kwake ni ufisadi na kukabiliana na matukio maovu, dhiki zote hizi zinamsababisha matatizo ya nafsi huenda zukampelekea yeye katika baadhi ya kuwa na tabia mbaya.

**Tatu: Kuathirika na mazingira yaliyo haribika**

Njooni tuangalie tupo katika mazingira gani tunayoishi? Na tunavuta pumzi kwenye hewa gani?

Mwanaadamu huathirika mara nyingi na mazingira anayoishi. Ikiwa ataishi katika mazingira yaliyo safi basi ukurasa wake wa nafsi huwa mweupe na safi na kusalimika. Ama mazingira hayo yakiwa yametandwa na maovu na machafu basi hilo huwa ni miongoni mwa sababu za kuharibika na kukengeuka.

Hakika mambo ya kibinafsi na utamaduni uloenea, na njia za usambazaji (*Mass media*) yote haya ni matamshi ya vile vitu vinavyomzingira mwanaadamu na kumuathiri.

Na hapana shaka kwamba mambo mingi ya uharibifu yamepenya kupitia mambo haya katika jamii yetu. Ambayo yanamfanya mmoja wetu kuwathirikika nayo asipokuwa macho na kuwa chongo na iwapo hatajiandaa na kutokuwa na matendo mema.

**Nne: na la mwisho: Kazi ya shetani**

Hakika kuwepo kwa muumin katika zama hizi kunazua tatizo kubwa kwa shetani. Je litakuwaje tatizo hilo iwapo muumin atakuwa anabeba ujumbe na kuongoza wengine na kuzifuta mbinu za shetani na kuvunja mazingira yake?

Hakika muumin aliyebeba ujumbe kwa wengine ndiye mtu wa hatari zaidi anayepigwa vita na shetani a kumfanyia kila juhudi. Na muumin huyo akighafilika kidogo tu shetani huwa yuko tayari kwa kuitumia fursa hiyo kupenyea kwenye maisha yake hata kama ni mwanga mdogo na kupitia madhambi madogo.

Kwa ajili hiyo imekuja katika Hadith tukufu kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, mwanachuoni mmoja ni tisho kubwa kwa shetani kuliko watu elfu wenye kufanya ibada, kwa sababu mwenye kuwabudu hufanya kwa ajili ya nafsi yake pekee na mwanachuoni hufanya kwa ajili ya kuelimisha wengine." (***Mizanul Hikma Juz*** 6 Uk. 461)

Na sababu iko wazi. Ni kwamba watu elfu wanaoabudu hawana muongozo mzuri katika dini na shetani huwa hapati taabu kubwa katika kuwapotosha. Ama muumini mmoja mwenye ufahamu mzuri wa dini yake kupotezwa na shetani huwa ni vigumu hii ni moja . Pili yeye ni kiungo kinachokabiliana na kuwathiriwa kwa kuongoza wengine.

Na hapo shetani anafanya kila juhudi juu ya kukipotosha kiungo hiki. Nacho ni muumini mwenye kubeba ujumbe kwa wengine. Na yametueleza mafundisho ya dini kutoka kwa mitume na maimamu wa uongofu wakitutahadharisha kutokana na kughafilika na kutusisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na tahadhari kila wakati.

Amesema kiongozi wa waumini (a.s.): "Na mwenye kughafilika ughuriwa na tamaa, na kufikiwa na harasa." (***Safinatul Bihar Juz*** 2 Uk. 323)

Na kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.): "Ikiwa shetani ni adui kwa nini tunaghafilika?" (***Safinatul Bihar Juz* 2 Uk. 323)**

**Tahadharini na maelekezo ya shetani**

Kuna jambo jengine la muhimu zaidi kwenye sehemu hii pindi shetani anapotaka kumpotosha muumin kutokana na njia iliyonyooka. Huenda asimkabili kupitia maovu na machafu yaliyowazi kwa mfano: Haanzi kwa kumshawishi anywe mvinyo, uliwati au kuwacha Swala. Haya ni mambo yenye kumfedhehesha muumin na ya kumfanya aonekane ameshindwa kujimudu. Kwa hiyo ni lazima shetani atafute njia muafaka anayowezea kumnasa muumin pindi tu anapoghafilika na kujisahau. Anasema kiongozi wa waumini

(a.s.) katika kumuusia Kumayl bin Ziyad: "Hakika miongoni mwao (mashetani) muna wenye kuhadaa, wenye kupambia watu maovu, wenye kuzitia nyoyo wasiwasi na wenye kutia kibri juu ya mtu kwa kadri ya uchaji Mungu wake au utendaji wake maovu kwa kutosheka na hayo humtawala mwanaadamu na kumshinda." (***Baswair wa hudaa* Uk. 62**) Basi ni upande gani anaoingilia shetani?

Yeye humjia muumin kupitia dini yake. Humtia fikra na maelekezo yenye kuhitilafiana na tabia ya dini. Kisha humpambia kwa nje kuwa aone hiyo ni ibada na uchaji Mungu. Na zinapoondoka kwa muumin tahadhari zake na mazingatio basi huingia katika mtego wa shetani na huwa ni katika mawindo yake.

Na haya ndiyo yaliyotahadharishwa na Qur'an pindi Mwenyezi Mungu (S.W.T..) aliposema "Wala msichanganye uongo na ukweli."

Na anasema kiongozi wa waumini (a.s.): "Kama uongo ungekuwa umeepukana na kuchanganyika na ukweli wasingehofiwa watu kwa kuritadi, na kama kweli imeepukana na kuchanganyika na uongo zingekoma ndimi za wapinzani wetu, lakini huchukuliwa fungu huku na fungu kule yakachanganywa (kweli na uongo) hapo ndipo shetani huwatawala watu wake na huokoka wale ambao wamepata uongofu kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.)." (***Nahjul Balagha Khulba*** Na. 50)

Na kwa namna hii ndivyo anavyotia shetani katika nyoyo za waumini kwa kuzidisha mambo ya dini na mengineyo kwa jumla.

Anasema Imam Zainul-Abidina Ali bin Husein (a.s.) katika maombi yake: "Lau kama shetani hawahadai wao juu ya kufuata maamrisho yako, asingekukosa wewe mtu yoyote. Na lau kama hakuwafanyia wao upngo kuuona kuwa ni kweli asingelipotea mtu yoyote katika njia yako iliyonyooka." (***Sahifa Sajjadiyy***. Dua Na. 37)

Kwa kufanya ibada, kusali, na kuomba ni kama jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na kudumu chini ya neno la uchaji Mungu ataishi muumin kwa kunyenyekea na kusalimika na uongo.

Hakika mfano wa mambo yale tuliyoyataja mara nyingi huwa ni mitego ya shetani anawawinjia baadhi ya waumini wakati wanapoghafilika.

## WADHAMINI JUU YA KUWA NA MSIMAMO THABITI

Na sasa: Na wapi hao wadhamini ambao anawaelekea mwanaadamu kwa kukabiliana na hatari ya kukengeuka na kupotea?

Jibu: Wadhamini hao ni: Kutanabahi sana, kuwa macho na kuipiga vita nafsi kutokana na maovu. Na ili mwanaadamu awe pamoja na hayo, hapa na lililo bora zaidi kama kujifunza kutoka kwa miongozo na wasiya wa viongozi waliongoka na babu yao mtukufu (s.a.w.).

Hiyo ni miongozo inayoingia ndani ya nafsi ya mwanaadamu ili kumpa muangaza asije akateleza katika nafsi yake na kuwa katika malezi na mazingira machafu.

Na wasia huu unampa mwanaadamu uwezo mkubwa wa nafsi ilikukabili ana na matatizo yaliyopo mbele ya muumini anaeshikamana na nafsi iliyo na matumaini.

Na mwisho, hakika muongozo huu unambainishia mwanaadamu kila mbinu za shetani na maelekezo yake. Na kumfanya mwanaadamu awe macho na tahadhari anapofuata njia iliyonyooka.

Hakika huu ni wasia mkubwa usioweza kukadiriwa na thamani ya kitu chochote. Umeletwa kwa viumbe kupitia viongozi waliojuwa maisha kwa uhakika na undani. Na wakampasulia mwanaadamu mbele yake njia ya msimamo na mafanikio. Ndipo wakapigiwa mfano mzuri katika kuwa madhubuti juu ya njia ilyonyooka mbali na matatizo yaliyokuwepo. Hakika huo ni wasia wa kweli unaotoka kwa viongozi waaminifu walokuwa na ikhlas. Umetoka ndani ya nyoyo zao ili uingie ndani ya nyoyo ya kila muaminifu mwenye ikhlas.

Ni haja ilioje juu ya kila muumin kuufuata wasia hu ili uwe ni kama miwani ambayo anayoonea nayo mbele yake maisha na matukio yote. Na ili uwe wasia huo kama uongozi kwake yeye

wa kumpelekea kwenye njia iliyonyooka na yenye mafanikio.

Hebu sasa tutazame baadhi ya wasia hiyo iliyo na maongozo makubwa.

**Miongoni mwa wasia wa Mtume (s.a.w.)**

Imepokewa kwenye wasia wake mkubwa uliokusanya muongozo kwa Abu Dharri al-ahifary (r.a.)

-Ewe Abu Dharri, yafuate ninayokuusia utakuwa bwana duniani na Akhera.

-Ewe Abu Dharri, patiliza mambo matano kabla ya kufikwa na matano haya mengine: ujana kabla ya uzee, uzima wako kabla ya maradhi, utajiri wako kabla ya umasikini, faragha yako kabla huja kuwa na shughuli na uhai wako kabla ya mauti.

-Ewe Abu Dharri, tahadhari na kuhairisha mambo, wewe ni wa ile siku uliyo nayo wala si wa ile siku ijayo, na siku ya pili ikikufikia ichukulie kama unavyoichukulia siku hii ya leo. Na siku ya pili isipokupata hutajuta kwa yale uliyoyafanya siku ya leo.

-Ewe Abu Dharri, wangapi wanaoingiliwa na siku na wasiimalize, na wakasubiri siku ya pili lakini isiwafikie (wakafariki).

-Ewe Abu Dharri, kKuwa bakhili kwa umri wako (tumia kwa tahadhari) kuliko kwa pesa zako na mali yako.

-Ewe Abu Dharri, Mwenye kutaka elimu kwa ajili ya kuhadaa watu haipati harufu ya Pepo.

-Ewe Abu Dharri, watu wa Peponi watawatokea watu wa motoni na kuwauliza: Ni lipi lililowaingiza motoni? Na hali sisi tumeingia Peponi kwa ajili ya muongozo na elimu yenu! Watasema watu wa motoni: Tulikuwa tunaamrisha mema wala hatuyafuati.

-Ewe Abu Dharri, wachaji Mungu ni mabwana, na wanazuoni ni viongozi na kukaa nao ni ziada, hakika muumin huona kosa

lake kama mawe na kuogopa yasimuangukie. Na kafiri huona kosa lake kama nzi aliyempitia puani mwake.

-Ewe Abu Dharri, hakika Mwenyezi Mungu (S.W.T..) akimtakia mja kheri humletea makosa yake mbele ya uso na kuyaona mazito makosa hayo.

-Ewe Abu Dharri, usiangalie udogo wa kosa bali angalia ni nani uliyemkosea. (***Biharul Anwar: Majlisi Juz* 77 Uk 74 - 91)**

**Miongoni mwa wasia wa kiongozi wa waumini (a.s.)**

Katika wasia uliokusanya miongoni anamuusia kiongozi wa waumini Ali bin Abi Talib (a.s.) Kumayl bin Ziyad (r.a.):

-Ewe Kumayl, hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amemfunza Mtume (s.a.w.w) adabu njema na yeye (s.a.w.) amenifunza mimi, na mimi nawafunza waumini.

-Ewe Kumayl, hakuna jambo lolote ila unahitajika kulifahamu.

-Ewe Kumayl, usimrejeshe patupu anayekuomba msaada mpe hata kama ni kipande cha zabibu au ganda la tende kwani sadaka ni yenye kumea.

-Ewe Kumayl, hakuna makosa kwa kutojulikana siri yako.

-Ewe Kumayl, Muumini ni kioo cha Muumin mwengine kwa sababu hujiangalia kwa makini na kujirekebisha na kujipamba.

-Ewe Kumayl, Shetani atakapoushawishi moyo wako basi sema: Najilinda kwa Mwenyezi Mungu mwenye nguvu kutokana na shetani mpotovu, na najikinga kwa Muhammad aliyeridhiwa kutokana na ubaya uliokadiriwa na kupitishwa, na najilinda kwa Mola wa watu kutokana na majini na watu waovu. Dua hii inatosha kuzivunja mbinu za Iblisi na mashetani ijapokuwa wote ni maibilisi.

-Ewe Kumayl, hakika miongoni mwao (mashetani) muna wenye kuhadaa, wenye kupambia watu maovu, wenye kuzitia

nyoyo wasiwasi na wenye kutia kibri juu ya mtu kwa kadri ya uchaji Mungu wake au utendaji wake maovu. Kwa kutosheka na hayo humtawala mwanaadamu na kumshinda.

-Ewe Kumayl, hakuna mwenye kutenda uadui kuliko wao (mashetani) wala mwenye kukudhuru wewe kuliko wao. Lengo lao ni kutaka uwe nao pamoja kesho watakapokuwa kwenye adhabu.

-Ewe Kumayl, umuhimu sio kuswali, kufunga na kutoa sadaka, umuhimu ni kutekeleza Swala kwa moyo safi, na vitendo viwe ni vyenye kuridhiwa na Mwenyezi Mungu, na uchaji Mungu sawa sawa na kuendelea kufanya bidii juu ya mambo hayo. (***Tuhajul Nquul: Al-Haram*** **Uk. 119 - 123**)

**Miongoni mwa wasia wa Imam Hasan bin Ali (a.s.)**

Alimwambia Junada bin Abi Umayya alipokuwa katika maradhi yake yaliyomfisha: "Nipe mawaidha ewe mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.). Imam Hasan bin Ali (a.s.) akamwambia sawa.

Jiandae kwa safari yako, na ukusanye zawadi zako kabla ya kufa kwako. Na ujue ya kwamba wewe unaifuata dunia na mauti yanakufuata wewe, wala usijihusishe na mambo ya siku ijayo kwa siku uliyo nayo. Na ujue ya kuwa : Duniani mambo yake ya halali ni hesabu na mambo yake ya haramu ni adhabu na katika mambo, na kuwa na dhana ovu ni lawama, Basi ifanye dunia ni kama maiti na uchukue kile kinachokutosha. Ikiwa ni halali basi huwa umeipa nyongo dunia, na ikiwa utachukuwa haramu basi ni kama uliechukuwa kitu katika mzoga, na likiwa ni lenye lawama basi lawama au makemeo ni mepesi. Na ufanye mambo ya duniani kana kwamba utaishi milele, na ufanye kwa ajili ya Akhera kana kwamba utakufa kesho.

Na ukitaka utukufu bila ya kusaidiwa na kabila na kuogopewa bila ya kuwa na ufalme basi jitoe kutoka katika machafu na ulekee kwenye kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu. **(*Qaadatuna Kayfa naakifuhuni: Al-Milani Juz.* 5 Uk. 325-326)**

## Miongoni mwa wasia wa Imam Muhammad Baqir (a.s.)

Katika kumuusia mmoja wa wanafunzi wake Jabir bin Yazid Al-Jaafy, Anasema (a.s.): "Nakuusia kwa mambo matano: Ukidhulumiwa usidhulumu, wakikuhini usiwahini, ukidanganywa usikasirike, ukisifiwa usifurahi na ukikejeliwa usiwe na huzuni na uyatafakari yale uliyoambiwa. Na yakiwa ni ya kweli yale uliyoambiwa basi kuonekana na Mwenyezi Mungu umekasirika kwa sababu umeambiwa kweli ni msiba mkubwa sana kwako kuliko yale unayoogopa usionekane na watu. Na yakiwa yale uliyoambiwa juu yako sio kweli basi hizo ni thawabu ulizozipata bila ya kuusumbua mwili wako.

Na ufahamu ya kuwa huwezi kututawala sisi mpaka wakusanyike watu wa mji wako na wakwambie: wewe ni mtu muovu kisha lisikuhuzunishe hilo, na lau watakwambia: wewe ni mtu mwema lisikufurahishe hilo. Lakini ilekeze nafsi yako katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na ukiifuata njia ya Mwenyezi Mungu kwa kuvipa nyongo vile alivyosema tuvipe nyongo, kupenda mambo ayapendayo, kuyaogopa yale aliyoyakhofisha, ukifanya hayo basi kuwa thabiti na uwe na bishara njema. Kwani hayatakudhuru wewe yale yasemwayo juu yako. Na ukiwa ni mwenye kuibaini Qur'an basi ni kitu gani kinachoighuri nafsi yako?

Hakika muumin ni mwenye kujitaabisha kwa kupigana na nafsi yake ili aishinde katika matamanio. Mara nyingine hujiweka sawa na kukhalifu matamanio yake kwa ajili ya kupenda Mwenyezi Mungu (s.w.t.), na mara nyingine hushindwa na matamanio na kuyafuata. Kisha Mwenyezi Mungu humzindua naye akazinduka, kisha huzingatia na kufanya toba na kuwa na hofu na huzidi kuwa muangalifu na ujuzi zaidi. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu amesema: "Wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu zinapowagusa pepesi za shetani mara hukumbuka, tahamaki wamekwishaona njia." (***Al-Aaraf* 201**). (***Tahaful Uquul* Uk. 206 - 207**)

**Miongoni mwa wasia wa Imam Jafar Sadiq (a.s.)**

Mambo muhimu na ukweli mkubwa anautoa Imam Sadiq (a.s.) katika kunuusia mmoja kati ya rafiki zake wa karibu (Abdallah bin Jundub Al-Kuufi). Tunachukuwa baadhi ya wasia huo kama ufuatavyo:

"Ewe mtoto wa Jundub, ni sawa juu ya kila Muislamu ayatazame matendo yake kila usiku na mchana kisha aihesabu nafsi yake, akiona ni mema basi aendelee, na akiona ni maovu aombe toba ili asije akahasirika siku ya Kiyama, furaha ni kwa yule mja aliyetafuta Akhera na kuitendea kazi.Furaha ni kwa yule asiyeghurika na matamanio ya uovu."

Kisha akasema (a.s.): "Mwenyezi Mungu awarehemu watu waliokuwa ni kama mwanga kwetu sisi, waliotulingania kwa amali zao sio kama yule mwenye kueneza siri zetu.

Ewe kijana cha Jundub, hakika waumini ni wale ambao wanamcha Mola na wana mori wa kufuata yale waliyopewa katika kuongoka, anapotajiwa Mwenyezi Mungu huwa na hofu na kuogopa. Na wanaposomewa maneno ya Mwenyezi Mungu Imani yao huzidi na wakawa wanamtegemea Mola wao.

Ewe kijana cha Jundub, ameangamia mwenye kutegemea amali yake, na mwenye kuyafikiri madhambi yake na kuwa na hakika ya kupata rehma ya Mwenyezi Mungu."

Nikamuuliza, basi ni nani atakayeokoka?

Akasema: "Ni wale walio baina ya matumaini ya kufaulu na kuogopa, kama kwamba nyoyo zao ziko kwenye makucha ya ndege, haya ni kwa ajili ya kutaka thawabu kuhofia adhabu."

-Ewe kijana cha Jundub, mwenye kutaka aozwe Hurul-ain na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na avishwe taji la nuru basi na amfurahishe nduguye Muislamu.

-Ewe kijana cha Jundub, punguza kulala usiku na mazungumzo yako mchana, kwani hakuna kiungo mwilini

chenye shukrani chache kuliko jicho na ulimi (kisichotosheka) kwani mama yake Suleiman alimwambia Suleiman (a.s.): "Ewe mwanangu, jitahadhari sana na kulalalala kwani jambo hilo litakutia ufukara siku ambayo watu watakuwa wanazihitaji amali zao."

-Ewe kijana cha Jundub, Hakika shetani ana mawindo na mitego, basi yakwepe mawindo yake na mitego.

-Ewe kijana cha Jundub, Mwenye kuenda kwa ajili ya kumtekelezea mwenzie haja ni kama aliyefanya *sa'ayi* baina ya Swafaa na Marwa, na akimtekelezea haja yake ni kama aliyemwaga damu yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu siku ya vita vya (Badr) au (Uhud). Na Mwenyezi Mungu haadhibu watu ila kwa sababu ya kusahau haki za ndugu zao walio mafukara.

-Ewe kijana cha Jundub, madhambi yote ni yenye kusamehewa isipokuwa kosa la kuwadharau watu wanaokulingania katika njia ya sawa. Na wema wote ni wenye kukubaliwa ila uliofanywa kwa ajili ya kuonesha watu.

-Ewe kijana cha Jundub, ukitaka kuwa jirani na kipenzi katika makao yake, na kuingia Pepo ya Firdaus karibu na yeye, basi ipuuze dunia na wala usitundize kitu kwa kesho. Na ujue kuwa yako ni yale uliyotanguliza na utaulizwa kwa yale uliyoyaacha.

Isubirishe nafsi yake kwa kila mtihani, ima wa watoto au mali au msiba, kwani Mwenyezi Mungu huvitwaa vile alivyokupa ili akujaribu kama ni mwenye kusubiri na kushukuru. Na utarajie mema kwa Mola matarajio ambayo hatakupeleka katika kumuasi, au umche kwa khofu isiyokukata tamaa kwa kupata Rehema zake (s.w.t.).

Wala usighurike na maneno ya wajinga, na wala asikusifu ukawa na kibri na kujifahari kwa vitendo vyako, kwani amali iliyo bora ni kumuabudu Mwenyezi Mungu na huku ukinyenyekea.

-Ewe kijana cha Jundub, usitoe sadaka mbele ya watu ili wakuone kuwa ni mwema, kwani ukifanya hivyo huwa umeufuta ujira wako. Lakini utakapotowa kwa mkono wa kulia basi wa kushoto usijuwe, kwani yule utakaempa kwa siri ulimwenguni atakulipa mbele ya mashahidi siku ambayo haitodhuru kutoa sadaka mbele ya watu (Kiyama).

-Ewe kijana cha Jundub, wema wote upo mbele yako, na uovu wote upo mbele yako. Na wala hutauona wema wala uovu ila baada ya Akhera. Kwa sababu Mwenyezi Mungu imeziweka kheri zote Peponi na maovu yote motoni, kwa sababu ni vitu vyenye kubaki milele. Basi ni wajibu kwa yule aliyefunguliwa na Mwenyezi Mungu uongofu, imani, na kuifanya akili yake itambue neema, na akampa elimu na hekima azingatie mambo ya dini na dunia. Mtu huyo anapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu wala asimkufuru, na amtaje Mwenyezi Mungu bila ya kumsahau na afuate maamrisho yake wala asimkosee.

Ama pindi kitakaposimama Kiyama na akaweka Mwenyezi Mungu mizani kwa ajili ya malipo. Na watu watakapoletewa kwa ajili ya malipo. Itabainika wakati huo ni nani atakayepata utukufu na kukirimiwa na ni nani atakaeangukia kwenye majuto.

Basi tenda wema hapa duniani ili ukapate yale uliyoyatarajia kesho Akhera.

-Ewe kijana cha Jundub, Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema katika mambo aliyomletea wahyi Mtume (s.a.w.). Hakika mimi ninaikubali Swala ya yule mwenye kunyenyekea kwa ajili ya utukufu wangu, na akaizuia nafsi kwa maovu kwa ajili yangu, na akautumia mchana kwa kunitaja wala hatakabari juu ya viumbe vyangu. Akamlisha mwenye njaa, na akamvisha aliye tupu, na akamuhurumia mwenye matatizo, na akampokea mgeni. Basi mtu huyo itang'ara nuru yake mfano wa Jua, na nitamuekea kwenye giza mwangaza, na kwa asilolijuwa upole. na nitamlinda kwa utukufu wangu na

kuwamrisha Malaika wamuhifadhi. Akiniita nitamuitikia na akiniomba nitampa. Mfano wa mtu huyo ni kama Pepo ya Firdaus hayaishi matunda yake wala hayaharibiki. (***Tuhaful Uquul*** **Uk. 221 - 226)**

**Katika wasia wa Imam Musa Al-Kadhim (a.s.)**

Ni wasia mzuri ulioje ambao anautoa Imam Al-Kadhim (a.s.) kwa mmoja wa wanafunzi wake watukufu Hisham bin Hakim Al-Baghdadi, hakika umebeba thamani iliyo juu kabisa hebu tufaidike na baadhi ya wasia hii:

-Ewe Hisham, kila kitu kina dalili na dalili ya akili ni kutafakari.

-Ewe Hisham, mkononi mwako mkiwa mna njugu, na watu wakakwambia, mkononi mwako mna lulu, haitokunufaisha ilihali wewe unajuwa kuwa ni njugu; na lau kama mkononi mwako mna lulu na watu wakakwambia ni njugu usingejali ilihali wewe unajuwa kuwa ni lulu.

-Ewe Hisham, hakika Mwenyezi Mungu ana hoja mbili kwa watu: Moja iko nje na wazi, na moja iko ndani. Ama ile iliyo wazi ni Mitume na Manabii pamoja na viongozi (Maimamu) na iliyo ndani ni akili.

-Ewe Hisham, mambo machache yaliyofanywa kwa akili ni yenye kuzidishiwa ujira na kukubaliwa. Na mambo mengi yanayofanywa na watu wa matamanio na wajinga hayakubaliwi.

-Ewe Hisham, ukiwa unaridhika na kile upatacho, basi kilicho karibu yako katika dunia kitakutosheleza. Na ukiwa hutosheki na kile upatacho basi hakuna kitu kitakacho kutosheleza duniani.

-Ewe Hisham, hakika wenye akili waliwacha ubora wa dunia vipi hawataacha madhambi. Kuacha dunia ni katika ubora na kuwacha madhambi ni katika wajibu.

-Ewe Hisham, hakika wenye akili wameipa nyongo dunia na wakaitaka Akhera. Kwa sababu walijua kuwa dunia ni yenye

kutafuta na kutafutwa na Akhera vile vile. Basi anayeitafuta Akhera dunia humtafuta yeye mpaka akapata riziki yake. Na mwenye kuitafuta dunia basi Akhera humtafuta yeye mpaka imleteee mauti na kuharibu dini yake na Akhera yake.

-Ewe Hisham, hakika Mwenyezi Mungu amenukuu kutoka kwa watu wema kwamba wamesema "Mola wetu usizipotoe nyoyo zetu baada ya kutuongoza na utupe rehema itokayo kwako, hakika wewe ndiwe mpaji mkuu." Pindi walipojua kuwa nyoyo hupotoka na kurudi katika maovu.

-Ewe Hisham, hana dini asiyekuwa na adabu, na hana adabu asiyekuwa na akili. Hakika mwenye uwezo mkubwa ni yule asiyeona dunia kuwa ni hatari kwa nafsi yake. Hakika miili yenu haina thamani ila kwa Pepo tu basi msisingizie kitu kingine.

-Ewe Hisham, hakika mwenye akili haongei na mtu anayehofia kuwa atamdanganya, wala hamuombi yule anaejuwa kuwa atamnyima, wala hashindani na asiyemueza, wala hatamani kitu kitakacho vunja matarajio yake, wala hafuati jambo ambalo litamshinda baadaye.

-Ewe Hisham, Mwenyezi Mungu amemrehemu yule mwenye kumuonea haya kihakika, akihifadhi kichwa chake na vile alivyovimiliki, na tumbo na linachokibeba, na akakumbuka mauti na mwisho wake. Na ujue kuwa Pepo imezungukwa na mambo yachukizayo na Moto umezungukwa na mambo yapendezayo.

-Ewe Hisham, Mewnye kuizuia nafsi yake kwa kutoharibu utukufu wa mtu, Mwenyezi Mungu atamsamehe siku ya Kiyama. Na mwenye kuzuwia hasira zake kwa watu, basi Mwenyezi Mungu atazizuia hasira zake kwake yeye siku ya Kiyama.

-Ewe Hisham, mwenye akili hasemi uongo hata kama ni kwa ajili ya matamanio yake.

-Ewe Hisham, zitengeze siku zako zilizo mbele yako. Itazame ni siku gani iliyokukabili na ujiandae na jawabu kwani

utasimamishwa na kuulizwa siku ya Kiyama. Na uchukuwe mawaidha kutoka katika ulimwengu na walimwengu, kwani maisha ni marefu na ni mafupi. Na utende wema kana kwamba unayaona malipo yake ili uwe na matumaini zaidi, na ujifunge kwa Mwenyezi Mungu, na utazame katika kugeuka ulimwengu na hali zake kwani yale yajayo katika dunia ni kama yale yaliyopita, basi yataka uzingatie.

-Ewe Hisham, watu wote huona nyota lakini hakuna inayemuongoza ila wale wenye kujua njia zake na makalio yake (*Manazil*). Vilevile nyinyi mnajifunza elimu lakini hakuna anaengoka nayo ila wale wenye kuifanyia kazi.

-Ewe Hisham, ni mtu muovu aliyoje mwenye nyuso na ndimi mbili, humfurahikia anapokutana naye na humsengenya anapompa kishogo. Anapopewa neema na Mwenyezi Mungu, humhusudu na anapopatwa na mitihani humtenga.

-Ewe Hisham, mtu hawi muumini mpaka awe ni mwenye khofu na matarajio ya mema. Na hawi mwenye khofu na matarajio mpaka ayaepuke yale anayoyahofia na afanye kwa yale anayotarajia.

-Ewe Hisham, mfano wa dunia ni kama mfano wa nyoka asiyeweza kufanya jambo lakini tumboni mwake mna sumu yenye kuuwa, wanajihadhari naye wenye akili na wanamwendea karibu watoto na kumshika kwa mikono yao.

-Ewe Hisham, fanya subra katika kumtii Mwenyezi Mungu na usubiri kwa kujizuia kumuasi hakika dunia ni kama wakati, ule uliopita huwezi kupata furaha wala huzuni, na ule ambao haujafika huujui utakuwaje. Basi fanya subra katika ule wakati ulionao kana kwamba umeufurahia.

-Ewe Hisham, mfano wa dunia ni kama mfano wa maji ya bahari kila anapoyanywa mwenye kiu humzidisha kiu mpaka afe.

-Ewe Hisham, jiepushe na kibri kwani hataingia Peponi yeyote mwenye athari ndogo ya kibri katika moyo wake. Kibri

ni vazi la Mwenyezi Mungu basi atakayemvua atamtumbukiza Motoni kwa kiuso uso.

-Ewe Hisham, amesema Mtume (s.a.w.w.) "Mtakapomuona muumin amenyamaza msogeleeni karibu kwani huwa anatafuta hekima. Na muumin huwa ni mwenye kuzungumza kidogo na kutenda kazi sana. Na mnafiki ni mwenye maneno mingi na matendo kidogo.

-Ewe Hisham, Mwenyezi Mungu alimpa wahyi Nabii Daud (a.s.) ya kwamba "Waambie waja wangu ya kuwa wasimuweke baina yangu na wao mwanachuoni aliyefitiniwa na dunia atawazuia wao kunitaja mimi na kufuata njia ya mapenzi yangu. Hao ndio waovu katika waja wangu. Jambo la Kwanza nitakalolifanya kwao ni kutoa utamu wa mapenzi yangu katika nyoyo zao.

-Ewe Hisham, Mwenyezi Mungu alimpa wahyi Nabii Daud (a.s.) na kumwambia: "Ewe Daud! Tahadhari na uwaonye jamaa zako juu ya kupenda matamanio ya nafsi zao, kwani wale ambao nyoyo zao zimetundikwa kwenye matamanio ya ulimwengu, nyoyo zao zimewekewa kizuizi baina yao na mimi."

-Ewe Hisham, jiepushe na kibri na kujivuna na elimu yako, atakuchukia Mwenyezi Mungu na wala haitakusaidia wewe dunia wala Akhera baada ya kuchukiwa na yeye (s.w.t.). Na ishi kwenye ulimwengu kama yule mwenye kuishi katika nyumba ambayo sio yake bali anasubiri kuondoka wakati wowote. (***Tuhaful Uquul*** Uk. 283 - 297)

Sheikh Hassan bin Musa bin bin Sheikh Ridha Saffar, amezaliwa mnamo mwaka (1377 A.H.) huko mjini Qatif, Mkoa wa Mashariki, nchini Saudi Arabia. Alipohitimu kusoma katika Chuo cha Qur'an, alijiunga na Madrasa ya msingi ya Zainul-Abidin, kisha akajiunga na Madrasa ya Kati ya Amin mjini Qatif, na hivyo kuanza kutoa khutba za kidini katika mwaka 1388 (A.H.) (1968 A.D.).

Mnamo mwaka 1391 (A.H.) (1971 A.D.), alikwenda huko mjini Najaf, Iraq kwa ajili ya kuongeza elimu na baadaye alikwenda kuendelea zaidi kwenye Hawza ya Qum (Iran).

Kisha alijiunga na Madrasa ya Rasuulul-Akram nchini Kuwait, na hapo ndipo alipokuwa ni miongoni mwa viongozi wa mwamko wa kiislamu nchini humo.

Sheikh Saffar amesimamia taasisi nyingi za kidini katika pande nyingi duniani ikiwemo Saudia, Oman, Syria, Iran na Marekani.

Vilevile ameshiriki katika matangazo mengi kupitia kwenye idhaa na magazeti mengi duniani. Ameshiriki mikutano mingi ya kiislamu ikiwemo Mkutano wa vijana wa kiislamu Marekani, na mkutano wa Umoja wa kiislamu chini Iran, pia vikao juu ya fikra katika Saudia; pia mkutano wa mlingano wa kuwa karibu baina ya madhehebu, nchini Bahrain.

Ametoa vitabu zaidi ya sabini na vimetarumiwa katika lugha mbali mbali za kigeni.

Sheikh huchukuliwa kama ni mmoja kati ya watu wanaopenda kuzungumzia uhuru wa kuwapo kwa wingi wa kiitikadi, na juu ya uelewa wa uzalendo na pia kufikia kuwa na neno moja katika Uislamu.